SportPesa
TZS. 499,059,740
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mbaroni** madai kukutwa akichezea sehemu za siri mtoto miaka mitatu

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Septemba 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580707

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## KESI YA MBOWE

# Mawakili utetezi washtukia jambo

**Kila** mshtakiwa kutetewa na mwanasheria wake, shahidi adai watuhumiwa walipata mafunzo ukomando...

*Endelea ukurasa 2*



Freeman Mbowe

# Machinga waanza rasmi kuondolewa barabarani

UKURASA 2




Wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, wakiendelea na shughuli zao licha ya kuwapo bango lililowekwa na Manispaa ya Kinondoni la amri ya kutofanya biashara kwenye eneo la Mwenge, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 3

### AJALI COASTER YAUA WANNE FAMILIA MOJA

WATU sita wamefariki dunia na wengine tisa wamejeruhiwa baada ya gari aina ya Toyota Coaster walilokuwa wakisafiria kutoka Dar es Salaam kwenda Lundu, Nyasa mkoani...

UKURASA WA 4

### MUHIMBILI YABADILI CHEMBE ZA DAMU

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa mara ya kwanza imefanikiwa kumbadilisha chembe nyekundu za damu mjamzito mwenye ugonjwa wa selimundu. Huduma hiyo imeanza kutolewa nchini...

UKURASA WA 4

### MPASUKO WAIBUKA RAIS WA CWT KUSIMAMISHWA

MPASUKO ndani ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) umezidi kushika kasi baada ya baraza la taifa kumsimamisha Rais wake...

UKURASA WA 4

### NEMC YASHANGAA JENGO HALMASHAURI KUJENGWA BONDENI

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC), limeshangazwa na jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kujengwa...

# Hujuma mkakati mafuta ya kula

UKURASA 3

**MICHEZO** MKWASA AWAPA YANGA MCHONGO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA




Mgambo wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wakivunja banda la Chips lililojengwa na kuziba uchochoro eneo la Miyomboni jirani na benki ya CRDB juzi, kinyume na sheria za mipango miji. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mawakili washtukia jambo kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI Peter Kibatala amedai mahakamani kwamba wamebaini kuna mgongano wa kimaslahi kutokana na maelezo yanayodaiwa kutolewa na mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, yanayowataja washtakiwa wengine na kuwahusisha na kesi ya ugaidi inayowakabili.

Aliwasilisha madai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Makosa ya Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Mustapha Siyani wakati kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu ilipokuja kwa ajili ya kuendelea kusikiliza ushahidi wa shahidi wa pili katika kesi ndogo.

Wakili Kibatala aliomba kutambulisha mawakili wa washtakiwa, akitaja mawakili 11 wanamtetea mshtakiwa wa nne, Freeman Mbowe peke yake.

Aliwataja mawakili hao kuwa ni Kibatala, Michael Mwangasa, Michael Rugina, Alex Masaba, Gaston Garubimbi, Deogratias Mahinyila, Hadija Aron, Selemani Matauka, Ferdnand Makole, Evaresta Kisanga, Marie Mushi na Jonathan Mndeme.

Wakili huyo alidai mshtakiwa wa kwanza, Halfani Bwire, atawakilishwa na Wakili Nashon Nkungu na Jeremiah Mtobesya, mshtakiwa wa pili, Kasekwa atawakilishwa na John Mallya na mshtakiwa wa tatu atawakilishwa na Dickson Matata.

Kibatala alidai wamefikia uamuzi huo wa kila mshtakiwa kuwakilishwa na wakili wake baada ya kupitia kwa kina maelezo yanayodaiwa kutolewa na mshtakiwa wa pili, Kasekwa akiwa kituo cha polisi na kugundua yanawataja mshtakiwa wa kwanza, watatu na wanne na kuwahusisha katika kesi.

"Tumegundua kuna mgongano wa kimaslahi, tunataka kila mshtakiwa awakilishwe na wakili wake badala ya utaratibu wa awali ambapo jopo lilikuwa linawakilisha washtakiwa wote.

"Hili hatukuligundua mapema, ushauri wangu kila wakili aulizwe kama kuna haja ya kumwita tena shahidi wa kwanza kwa ajili ya kuhojiwa maswali," alidai Kibatala.

Jaji Siyani aliwahoji mawakili pamoja na washtakiwa wote kama wanahitaji kumhoji maswali shahidi wa kwanza lakini wote walikataa, wakaruhusu mahakama iendelee kusikiliza ushahidi wa shahidi wa pili.

Alisema hayo ni mambo ya kisheria yanayohusu haki za watu, hivyo kila hatua inatakiwa kuzingatia misingi ya kisheria.

"Kwa upande wangu, ninahitaji kutafakari kuamua kwamba tuendelee au shahidi aitwe kuhojiwa, ninajipa dakika chache za kutafakari," alisema. Baada ya dakika 15, Jaji Siyani aliingia na kusema kwamba Septemba 15, mwaka huu wakati Kibatala akiwasilisha pingamizi, alijitambulisha kwa niaba ya mawakili wote na washtakiwa wote wanapinga kielelezo.

Alisema hoja na maswali yalikuwa kwa niaba ya washtakiwa wote, hivyo haoni sababu ya kumwita shahidi kwa kuwa washtakiwa walipata nafasi ya uwakilishi.

Mahakama iliruhusu shahidi wa pili, Inspekta Mahita Omary, kuanza kutoa ushahidi wa madai kwamba mshtakiwa wa pili, Kasekwa aliteswa kabla na wakati akichukuliwa maelezo.

Inspekta Mahita alidai alishiriki kuwakamata washtakiwa mkoani Kilimanjaro maeneo ya Rau madukani Agosti 5, mwaka 2020 na Agosti 7, mwaka huo waliwapeleka Dar es Salaam.

Alidai wakiwa safarini, walikuwa wakitoa nafasi kwa washtakiwa pamoja na askari kupata chakula, Agosti 8, mwaka huo aliitwa na ACP Kingai, akapewa maelekezo ya kuwatoa washtakiwa mahabusu Kituo cha Kati na kuwapeleka Polisi Mbweni.

Inspekta Mahita alidai waliwapeleka Mbweni kwa sababu ya mazingira ya kesi na kwamba walipata mafunzo ya ukomandoo.

Akihojiwa na Wakili Mallya alidai hafahamu kama ACP Kingai ana tatizo la kumbukumbu na anaamini atakachosema atakuwa yuko sawasawa. Alidai Kituo cha Polisi Mbweni hakina ofisi nyingi kama zilizopo Kituo cha Polisi cha Kati. Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kulipua vituo vya mafuta, masoko, kukata miti barabarani na kuwadhuru viongozi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA SHIRIKA LA UVUVI TANZANIA(TAFICO)**

Kufuatia uteuzi wa **Prof. Yunus Daud Mgaya** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) **Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki**, Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (The Public Corparation No. 17 of 1969} (The Tanzania Fisheries Corporation) (Establisment) order, 1974 , Tangazo la Serikali Na. 58 la tarehe 01/03/1974, amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)

1. Bw. Magesa Emmanuel Bulayi
2. Bw.Hamidu Rajab Mwanga.
3. Dr. Ismail Kimerei,
4. Bw. Said Meck Sadick,
5. Bi. Prisca Burton Lwangili,
6. Dkt. Eliamini Aloyce Kasembe,
7. Bw. Oscar Celestine Kibazohi,
8. Bw. Anthony Raphael Chayeka
9. Bw. Derick August Mushi
10. Bw. Japhet Justine

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe ya 17/09/2021 hadi 16/09/2024 Katibu Mkuu na Menejiment ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

Dkt. Rashid A. Tamatamah
KATIBU MKUU - UVUVI

216467902


# Machinga waanza kuondolewa barabarani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, imeanza kuwaondoa barabarani wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga na kuwahamishia maeneo rasmi kama alivyoagiza Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa kuanzia, manispaa hiyo imeanza kukagua miundombinu kwenye masoko yote, ili kuyarekebisha kabla ya kuanza kuwapanga machinga katika maeneo rasmi ya kufanyia biashara.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Masalla, baada ya kumaliza ziara yake ya kata zote 19 na kuitisha kikao cha majumuisho kilichowahusisha madiwani, wenyeviti wote wa mitaa, watendaji, walimu wakuu wa shue za msingi na sekondari .

Masalla alisema uongozi wa halmashauri hiyo, umeanza mchakato huku moja ya mikakati yao ni kutembelea maeneo yote ya masoko kujiridhisha kama kuna mahitaji muhimu ikiwamo maji na vyoo, ili kuweka mazingira bora kwa wafanyabiashara hao.

Alisema wananchi kufanya biashara holela ni tatizo wilayani hapa, hivyo wakati umefika kupanga maeneo, ili biashara zifanyike kwa kufuata utaratibu.

Mkuu huyo wa wilaya aliongeza kuwa, maeneo muhimu watakayoyatembelea kukagua miundombinu ni pamoja na soko la Kiloleli, Nyasaka, Kirumba, Sabasaba na Buzuruga .

Alisema ana imani kuwa kazi hiyo itafanyika kwa utulivu , amani na ushirikiano na kwamba hawatatumia migambo wala polisi na kwamba halmashauri hiyo, itakuwa ya mwisho kutumia nguvu kwa kuwa wamezungumza na viongozi na mazungumzo yanaendelea ili kuona ni gani kero wanazokutana nazo, ili wasaidiane kuzitatua.

Kwa upande wa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye pia ni Mbunge wa jimbo la Ilemela, Dk. Angeline Mabula, alisema awali kuwa kazi ya kuwapanga machinga kwenye maeneo yao ilienda vizuri na walihamia kwenye maeneo husika.

Dk. Mabula alisema bado ana imani kwa sasa kazi hiyo itafanyika vizuri kwa kuwa wafanyabiashara hao ni waelewa na wakishirikishwa wataenda, bila manung'uniko yoyote.

"Kazi hii awali ilifanyika vizuri, lakini alitokea mtu mmoja akampigia simu Hayati Rais John Magufuli na kumweleza machinga wameteswa na wamevunjiwa vitu vyao ndipo akaagiza warudishwe kwenye maeneo waliyokuwapo, hivyo niombe viongozi wote tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kazi hiyo, inaendea vizuri na kuisha kwa amani," alisema Mabula.

HABARI KITAIFA

# PM aonya hujuma mkakati utatuzi tatizo mafuta kula

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaonya baadhi ya wananchi katika Mkoa wa Kigoma, wanaohujumu zao la kimkakati la michikichi kwa kuchoma moto na kulisha mifugo.

Amesema huo ni uhujumu uchumi na kuwahakikishia Watanzania kuwa kilimo hicho muda si mrefu kitamalizia upungufu wa mafuta ya kula baada ya mbegu iliyofanyiwa utafiti aina ya TENERA kuanza kutoa matunda ndani ya miaka miwili na nusu.

Akizungumza juzi na wananchi wakati wa ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa maagizo yake kuhusu kuendeleza michikichi katika shamba la ekari 6,000 la Gereza la Kwitanga wilayani Kigoma, Waziri Mkuu alisema serikali itawachukulia hatua kali wale wote wanaofanya hujuma dhidi ya zao hilo. "Nimepita katika shamba la michikichi la Gereza la Kwitanga ambalo wamepanda zao hilo tangu mwaka jana lakini wananchi wamewasha moto na kuunguza shamba lote karibu asilimia 80. Sasa nawaonya hilo ni zao la kimkakati na tumeweka sheria kali sana isije ikakuangukia "

Waziri Mkuu alisema mbegu hiyo ya Tenera imeonyesha ina uwezo wa kuzalisha mafuta tani tano mpaka sita kwa hekta moja tofauti na mbegu ya zamani inayozalisha wastani wa tani 1.6 kwa hekta.

Pamoja na hujuma hiyo, Waziri Mkuu alisema kutokana na mafanikio ya mbegu hiyo, aliwataka wakulima wa zao hilo katika Mkoa wa Kigoma kuiondoa kwa awamu aina ya michikichi iliyopandwa kwa kutumia mbegu ya zamani inayoanza kuzaa baada ya miaka saba.

"Wakulima wa michikichi mmeliona hili shamba. Tumepanda mbegu ya Tenera mwaka 2019 lakini mpaka sasa ni miaka miwili na tayari imeanza kutoa matunda, hivyo nawaomba mpande hii mbegu mpya katika mashamba yenu huku mkitoa kwa awamu ile mbegu ya zamani aina Dura," alisema. Waziri Mkuu Majaliwa alipongeza Gereza la Kwitanga kwa kuamua kulima ekari 6,000 za michikichi kwa kuwa utakuwa mradi mkubwa wa jeshi hilo ambao utasaidia kuongeza mapato na kujitegemea.

Aliagiza uongozi wa gereza hilo kuongeza uzalishaji wa mbegu za Tenera na kuwapatia bure wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka gereza ili walime michikichi kwa kutumia mbegu ya kisasa.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo, alisema miongoni mwa maelekezo waliyopokea kutoka kwa Waziri Mkuu ni kuzalisha mbegu bora aina ya Tenera ambayo mpaka sasa wamezalisha zaidi ya mbegu milioni 3.5 na kuzigawa bure katika taasisi na halmashauri nane za mkoa huo.

Alisema maelekezo mwingine hao watu wanaopatiwa mbegu hizo wanapaswa kuzitunza na kuhakikisha zinaota kwa kuwa gharama za kuzalisha miche ni kubwa. Alibainisha kuwa mche mmoja gharama halisi ni Sh. 1,000.

Mkurugenzi huyo alisema katika maeneo mbalimbali waliyopita, wamegundua baadhi ya miche inaliwa na mifugo na mingine inachomwa moto kitu ambacho kinasababisha hasara kwa serikali.

Dk Mkamilo alisema miche kuliwa na wanyama au kuchomwa moto ni jambo lisilokubalika kwa sababu linaweza kurudisha nyuma mkakati wa nchi wa kuzalisha mafuta ya kula.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka Mkuu wa Gereza la Kwitanga wilayani Kigoma, Uswege Mwahesya (kulia), kuhusu mchikichi alioupanda mwezi Mei 23. 2020, alipotembelea shamba la michikichi la gereza hilo, mkoani Kigoma jana. Kushoto ni Mkewe Mary Majaliwa. **PICHA: OWM**

# Mbaroni tuhuma za kuchezea sehemu za siri mtoto miaka 3

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia Antony Lugendo (34) mkazi wa Mlandizi, Wilaya ya Kibaha, kwa tuhuma za kukutwa akiwa anamchezea mtoto sehemu zake za siri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema mtuhumiwa huyo alikutwa akifanya kitendo hicho, juzi majira ya saa 10:00 jioni, eneo la Kaloleni Kata ya Janga. Wankyo alisema mtuhumiwa huyo alikutwa chumbani kwake akiwa amemvua nguo zote mtoto huyo wa miaka mitatu huku akimchezea.

Alisema kwa sasa mtuhumiwa huyo anashikiliwa kwa taratibu za kisheria kwa tuhuma za kumdhalilisha mtoto huyo wa darasa la awali.

Katika hatua nyingine, Kamanda huyo alisema kwa kipindi cha wiki mbili, umefanyika msako wa kutokomeza uhalifu na watuhumiwa 38, wametiwa mbaroni pamoja na kuokoa mali za wananchi zilizokuwa zimebiwa.

Akizungumzia upande wa usalama barabarani, Kamanda Wankyo alisema makosa 3,971 yalikamatwa na faini za papo kwa papo za Sh. 119,130,000 zilikusanywa.

Wankyo aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wa kutoa taarifa za uhalifu, ili kufanyiwa kazi mapema.

# Ajali Coaster yaua wanne familia moja

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATU sita wamefariki dunia na wengine tisa wamejeruhiwa baada ya gari aina ya Toyota Coaster walilokuwa wakisafiria kutoka Dar es Salaam kwenda Lundu, Nyasa mkoani Ruvuma kuacha njia na kupinduka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 8.30 mchana huko katika kijiji cha Kipololo wilayani Mbinga.

Alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili T503 DWF aina ya Toyota Coaster mali ya Joseph Eugene mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Mohamed Athumani (37) ambaye alikuwa dereva wa gari hilo na mkazi wa Mbezi, Penzia Challe (60) mfanyabiashara na mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam, na Franko Challe (40) fundi magari mkazi wa Songea mjini.

Wengine ni Joyce Ndonde (45) muuguzi ambaye pia ni mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, Gerard Ndonde (60) mwalimu wa Shule ya Msingi Ruhuwiko, Manispaa ya Songea na Johnson Challe (11) mwanafunzi wa Shule ya Msingi na mkazi wa Dar es Salaam.

Kamanda Konyo aliwataja majeruhi kuwa ni Nathan Ndonde (60) mkazi wa Majumba Sita, Dar es Salaam, Geoffrey Challe (40) mkazi wa Banana, Dar es Salaam, Nelson Ndonde (40) mkazi wa Tabata, Amina Mpangala (34) mkazi wa Dar es Salaam na Janeth Ndonde (35) mwalimu wa shule ya msingi jijini Dar es Salaam.

Wengine, kwa mujibu wa Konyo, ni Janeth Ndonde (33) mfanyabiashara mkazi wa Tabata, Olivia Ndonde (36) mfanyabiashara mkazi wa Tabata, Catherine Ndonde ambaye ni muuguzi na mkazi wa Dar es Salaam na Patrick Mpangala (32) mkazi wa Tabata.

Alisema kuwa majeruhi hao wamelazwa katika Hospitali ya Misheni Litembo wilayani Mbinga ambako wanaendelea kupatiwa matibabu na miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbinga ikisubiri uchunguzi.

Konyo alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva wa gari hilo kwenye mteremko mkali wenye urefu wa zaidi kilomita moja bila kuchukua tahadhari ya kutosha na ugeni wa njia, hivyo gari kumshinda na kutumbukia kwenye bonde lenye urefu wa zaidi ya mita 120.

Kutokana na ajali hiyo, Kamanda Konyo aliwataka watumiaji wa vyombo vya moto kuwa makini kwa kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani ili kuepukana na ajari zisizo za lazima kwa maisha ya watumiaji wengine wa barabara na maisha yao wenyewe.

## NEMC yashangaa jengo Halmashauri kujengwa bondeni

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC), limeshangazwa na jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kujengwa eneo la Bonde la Mto Ruvu ambalo mvua ikinyesha hujaa maji.

NEMC imesema ujenzi huo haukufayiwa tathmini ya athari za mazingira na unaweza kusababisha uhaba mkubwa wa maji kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani siku za baadaye.

Hayo yalisemwa jana mkoani Pwani na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alipotembelea jengo hilo lililoko Mlandizi kujua sababu za kujengwa kwenye eneo oevu.

Dk. Gwamaka alisema eneo hilo ni miongoni mwa maeneo oevu ambayo ni hifadhi ya maji, hivyo shughuli yoyote ya ujenzi haipaswi kufanyika kwani inahatarisha kupungua kwa maji kwenye eneo hilo.

Alisema maji yanapojaa kwenye Mto Ruvu eneo hilo linakuwa kama hifadhi kwa kuwa maji yanapopungua kwenye mto yale yaliyoko chini kwenye maeneo hayo jirani hujichuja na kwenda mtoni.

Mwaka wa fedha wa 2011/12, alisema serikali ilitoa eneo kwa hilo kwa ajili ya kuendelezwa lakini kwa muda mrefu NEMC haikubaini kwamba linajengwa viwanda na majengo ya ofisi bila kufanya tathimini ya athari za mazingira. "Hili ni eneo oevu na katika sheria ya mazingira maeneo kama haya ni ya kulindwa kwa ajili ya kuhifadhi ikolojia ya eneo husika kwa sababu mabonde yanapanuka kwa ajili ya kuchuja na kuhifadhi maji. Ni kama sponji inahifadhi maji wakati wa mvua," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mito yote iliyopo si kwamba maji yalitengenezwa bali ni mfumo wa asili uliotengenezwa kiikolojia ambapo wakati wa kiangazi maji yanajichuja na kwenda kwenye mito kutiririka na binadamu kuyatumia.

Alisema maeneo hayo yanapovamiwa na kuendelezwa bila kufanyika tathmini ya athari za mazingira ni hatari kwani haijulikani nini kitatokea siku za baadaye na hasa ukosefu wa maji.

"Juzi DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam) walitangaza kwamba kina cha maji kimepungua, sasa kwa nini kimepungua na kwa nini mwaka huu. Bila shaka sababu ni kwamba ujenzi umekuwa ukiendelea kwenye maeneo haya oevu. Matokeo yake maji yanakosa sehemu ya kutuama na kuhifadhiwa kwenye haya maeneo na kiangazi tunakosa maji," alisema.

Alisema iwapo hali hiyo itaendelea kwa miaka 10 au 20 kuna hatari kwa Mkoa wa Dar es Salaam kukosa maji kwa sababu maeneo yote oevu yatakuwa yamejengwa na maji hatakosa sehemu ya kuhifadhiwa ardhini.

# Muhimbili yabadili chembe za damu

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa mara ya kwanza imefanikiwa kumbadilisha chembe nyekundu za damu mjamzito mwenye ugonjwa wa selimundu.

Huduma hiyo imeanza kutolewa nchini wiki hii kufuatia serikali kununua mashine mbili aina ya Spectra Optia zenye thamani ya Sh. milioni 245 ambazo zinatumika kutibu magonjwa zaidi ya 10 ukiwamo wa kupandikiza uloto.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu wa MNH, Dk. Mbonea Yonaz, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema awali matibabu hayo ya kumbadilisha mgonjwa damu yalikuwa wakiyafanya kwa njia ya kawaida kabla ya kupata mashine hizo.

Alisema mashine hiyo inatumia saa mbili hadi na nusu kubadili chembe nyekundu za damu wakati mfumo wa awali ulitumia hadi saa sita kutoa huduma kwa mgonjwa mmoja.

"Selimundu ni ugonjwa wa kurithi ambao mwathirika anakuwa amerithi vinasaba vya ugonjwa kutoka kwa wazazi wote wawili," alisema Dk. Yonaz.

Alifafanua kuwa chembe nyekundu za damu ni kibebeo au mabegi yanavyobeba wekundu wa damu ambayo husafirisha hewa safi ya oksijeni mwilini.

"Kasoro ya vinasaba anavyorithi mgonjwa husababisha kutengenezwa kwa wekundu wa damu (Haemoglobini) yenye kasoro inayojikunja na kusababisha chembe nyekundu kujikunja," alisema.

Alisema zaidi kuwa tatizo hilo huathiri hali ya ujauzito kwa kuharibu mimba changa, kujifungua mtoto mfu, kujifungua kabla ya wakati (njiti) na kujifungua mtoto mwenye uzito pungufu.

Dk. Yonaz anasema husababisha upungufu wa damu (Anaemia) wa kudumu unaoambatana na njano ya macho kutokana na kuvunjwa vunjwa kwa kasi chembe nyekundu za damu.

Alisema kwa kawaida mgonjwa huwa na Haemoglobini ya gramu saba hadi tisa wakati mtu asiye na ugonjwa anapaswa kuwa na kuanzia gramu 12 kwa wanawake na gramu 13 kwa wanaume.

"Chembe nyekundu za damu za kawaida zisizo na kasoro huishi kwa siku 120 ila za wenye tatizo hili hujikunja, hivyo kuonekana zimeezeekа na kuvunjwa vunjwa na kuondolewa ndani ya siku 15 hadi 20 tu," alifafanua.

Alisema dosari hiyo husababisha maumivu makali ya mara kwa mara, athari kwenye mifupa, kusagika na hatimaye kupata ulemavu, husababisha kiharusi kwa watoto wadogo na wenye Selimundu, huleta athari katika moyo, kuathiri utendajio wa figo, mfuko wa nyongo na vidonda vya miguu visivyopona.

Mtaalamu huyo alisema husababisha chembe nyekundu za damu zijikinge na kuwa na umbile la mwezi mchanga na kusabisha zisipite kwenye mishipa ya damu na kuleta dalili na athari zote za ugonjwa huo.

"Pamoja na matibabu ya kibobezi tuliyonayo, tunasisitiza kuwa wenye ugonjwa huu kusajiliwa katika kliniki maalum, kutumia maji ya kutosha kila siku kuanzia lita 3.5 na matumizi ya vitamin ya Folic Acid na dawa ya Hydroxyurea kila siku," Dk. Yonaz.

Mgonjwa wa Selumundu, Ester Raymond, alishukuru MNH kwa huduma hiyo ya kubadilishiwa damu kwa sababu maumivu yote yameisha, anajiona mzima na mwenye afya tele.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini, lililojengwa kwenye eneo oevu Mlandizi, Mkoa wa Pwani, bila kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mpasuko waibuka Rais CWT kusimamishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MPASUKO ndani ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) umezidi kushika kasi baada ya baraza la taifa kumsimamisha Rais wake, Leah Ulaya.

Rais huyo alisimamishwa kutokana na hoja 13 zilizowasilishwa na walimu wawili lakini baadhi ya wajumbe kuibua hoja zinazoonekana kuwagawa baadhi kuhoji inakuwaje Katibu Mkuu, Deus Seif, anaendelea kubaki madarakani.

Aliyekuwa mjumbe wa baraza hilo na Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Dodoma, Clement Mahemba, alijitokeza mbele ya vyombo vya habari jana na kusema kitendo kilichofanywa na baraza hilo ni cha uonevu dhidi ya Ulaya.

Mahemba alisema kutokana na hoja zilizotolewa na Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani, kuwa moja ya sababu ya kusimamishwa rais huyo ni ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CWT), kuondolewa kurasa zilizomtaja na kumtaka awajibike.

"Rais hana ofisi katibu mkuu ndiye mwenye ofisi, hivyo barua zote zinakwenda kwake kwa mujibu wa katiba. Kama kuna karatasi zilipotea kwenye ripoti ambazo zilikuwa zinamtaja Rais Leah Ulaya, inabidi wajiulize anayepoikea barua ni mwenye ofisi ambaye ni katibu mkuu," alisema.

Pia alisema katika hoja nyingine ambayo inadai kuwa rais huyo alishindwa kuwasemea walimu, ni mpango tu wa kumwangushia 'jumba bovu'.

"Wakati wa utawala wa hayati Rais John Magufuli, kama chama tulikubaliana kuwa hatutakuwa chama cha matamko bali tufanye kazi kwa kuipa ushirikiano serikali lakini nashangaa leo hii linakuwa kosa la rais. Hii siyo sawa.

"Rais hawezi kutoa tamko bila kuandikiwa na katibu mkuu na Rais anatoa tamko baada ya kuandaliwa na kamati. Yeye anatumika kwa ajili ya kusoma tuu, hizi hoja zao nafikiri ni sehemu tu ya kutaka kupoteza umakini kwenye kesi za msingi zinazowakabili viongozi ambazo ziko mahakamani," alisisitiza Mahemba.

Alisema kabla ya kuanza vuguvugu la kumwondoa katika nafasi hiyo, Seif aliandaa maombi ya mkopo wa Sh. bilioni 1.5 lakini benki ilikataa kutoa kiasi hicho na wakasema kutokana na sifa, wanapaswa kupewa bilioniSh. 1.1.

"Mkopo huu ulikuwa ni kwa ajili ya kuwalipa walimu wastaafu lakini baada ya benki kusema watatoa Sh. bilioni 1.1, rais alitia saini fomu za maombi. Baada ya muda kupita tena, katibu mkuu alileta fomu zingine za mkopo kama huo na rais akakataa kutia saini ndipo lilianza vuguvugu hili na kutaka kufanya mapinduzi ya kumwondoa katika nafasi yake," alisema Mahemba

Seif alipotafutwa, alisema kuwa yeye si msemaji wa chama, hivyo atafutwe kaimu rais ndiye atakaye toa ufafanuazi kuhusu suala hilo.

Hata hivyo, Mathamani alisema Ulaya hajafukuzwa bali amesimamishwa hadi hapo mkutano mkuu utakapofanyika mwakani.

"Mimi kama mwenyekiti nilipokea hoja kutoka kwa wajumbe ambazo zilijadiliwa na yeye rais akiwapo na kupiga kula ya kutaka kumsimamisha tena kura ya wazi. Kama kuna watu wanaona ameonewa basi nafasi bado anayo kwenye mkutano mkuu," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa hoja zinazolalamikiwa na wajumbe ni rais huyo kukaa kimya bila kutoa ripoti yoyote ya maendeleo ya chama. Kuhusu Katibu mkuu kuendelea kufanya kazi wakati akiwa na kesi mahakamani alisema kuwa katiba yao iko kimya katika suala hilo.

Juzi, kaimu rais huyo akizungumza na vyombo vya habari jijini hapa, azitaja baadhi ya hoja zilizofanya kusimamishwa kuwa ni kutengeneza mazingira ya kutofanyika uchaguzi kujaza nafasi ya katibu mkuu baada ya aliyekuwapo kufariki dunia.

# CCM yaipa 'tano' NHC

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KATIBU wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Shaka Hamdu Shaka, ametembelea mradi ujenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini Mtwara na kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kazi nzuri ya ujenzi wa jengo hilo la kisasa.

Akiwa katika ziara hiyo jana, Shaka alisema kuwa CCM inatambua kazi nzuri inayofanywa na NHC Taifa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho.

''Kwa niaba ya CCM nalipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi nzuri ya kupigiwa mfano ya ujenzi wa jengo la kisasa litakalosaidia kupunguza gharama kwa wananchi wa Kanda ya Kusini za kufuata huduma ya matibabu ya ngazi ya rufani jijini Dar es Salaam,'' alisema.

Shaka alisema kwa miaka mitano iliyopita NHC imekuwa kimbilio kubwa la CCM, katika utekelezaji mahiri na makini wa Ilani ya Uchaguzi na kwamba itaendelea kuliunga mkono shirika, ili kuwasaidia Watanzania wengi zaidi.

Hata hivyo, Shaka alisema hakufurahishwa na maandalizi ya kuanza utoaji wa huduma kwenye hospitali hiyo, iliyokamilika kwa asilimia 97 kama Wizara ya Afya ilivyomuahidi Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Wizara hiyo kupitia Naibu Waziri wake, Dk. Godwin Mollel, ilimhakikishia makamu wa rais, kuwa Hospitali hiyo ingeanza kutoa huduma mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu.

Kutokana na hali hiyo, Shaka aliiagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuacha urasimu na kuhakikisha inatekeleza ahadi yake ya kuanza kutoa huduma katika hospitali hiyo ifikapo Oktoba 2021.

"Sioni dalili yoyote ya kuanza utoaji wa huduma hapa, hakuna vifaa wala maandalizi ya muhimu ya kuanza utoaji huduma" alisisitiza Ndugu Shaka kwa masikitiko makubwa," alisema..

Naye Meneja wa NHC Mtwaa, Angeline Magazi, akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, alimweleza Shaka kuwa mradi huo utakaogharimu Sh. bilioni 15.8 hadi kukamilika umefikia asilimia 97 na kazi zinazoendelea zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba 2021, ambapo shirika litakabidhi jengo hilo.

# Waziri Mkuu amaliza mgogoro wa ujenzi ofisi za halmashauri

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amemaliza mgogoro juu ya sehemu ya ujenzi wa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na kuagiza ufanyike kwenye Kata ya Mahembe kama ilivyopendekezwa katika vikao vya baraza la madiwani.

Awali, kulikuwa na mvutano uliojitokeza baada ya wataalamu kupendekeza ujenzi huo ufanyike katika Kata ya Kamala.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana baada ya kusimamishwa na wakazi wa kata hiyo, ambao walidai uamuzi wa madiwani umebadilishwa na kusisitiza kuwa, kama sababu ni eneo kutofaa kwa ujenzi wa majengo ya ghorofa wabadilishe ramani, ili yajengwe ya kawaida. Wananchi hao, ambao waliwasilisha malalamiko yao kupitia mabango, walimweleza waziri mkuu, kwamba hawaridhishwi na uamuzi wa serikali wa kuhamishia ujenzi wa ofisi za halmashauri katika Kata ya Kamala wakati baraza la madiwani lilishatoa uamuzi kupitia vikao rasmi.

Baada ya kusikiliza malalamiko hayo, Majaliwa alimtaka Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchata, atoe ufafanuzi juu la suala hilo. Kiongozi huyo alikiri kuwa ni kweli ujenzi ulipendekezwa ufanyika katika eneo hilo, ila uamuzi wa kubadilisha ulitokana na ushauri wa wataalamu, ambao walisema eneo hilo halifai kujengwa majengo ya ghorofa, kama ramani inavyoonyesha.

"Kama eneo hili halifai kujengwa ghorofa ni lazima mjenge majengo ya ghorofa? Wananchi wanahitaji majengo ya kutolea huduma. Unajua uamuzi wa eneo la ujenzi yameamuliwa na wananchi kupitia baraza la madiwani, hivyo yazingatiwe huko msiende kujenga," alisema.

"Serikali iko makini na haiwezi kuwaangusha. Halmashauri itajengwa katika eneo lililochaguliwa na vikao vya baraza la madiwani na kama wataalamu watasema eneo hilo halifai kujengwa majengo ya chini waende kuhamisha kijiji maana patakuwa hapafai kwa makazi," alisisitiza.

Naye Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Assa Makanika, alisema baraza la madiwani lilipendekeza, kuwa ujenzi wa jengo la halmashauri katika eneo hilo na alishangaa kusikia ukihamishiwa katika eneo lingine, hivyo akaomba maombi ya wananchi yasikilizwe.

Pia Diwani wa Kata ya Mahembe, Mamisho Seif, alisema baraza la madiwani lilifanya vikao na kupiga kura kuamua eneo, ambalo zitajengwa ofisi za halmashauri na Kata ya Mahembe ilichaguliwa kati ya kata sita zilizopendekezwa.

"Jambo la kusikitisha ni kitendo cha wataalamu kufanya mabadiliko ya eneo la ujenzi na kuhamishia katika Kata ya Kamala. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba uamuzi wa baraza la madiwani ufuatwe," alisema.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kushoto), akiangalia ramani ya barabara ya juu 'Flyover' ya Chang'ombe, wakati alipotembelea na kukagua miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya barabara mkoani Dar es Salaam jana, ili kuona maendeleo yake. **PICHA MARY GEOFREY**

# Waganga wakuu kuwajibishwa usimamizi matumizi ya fedha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema itawawajibisha Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri watakaoshindwa kusimamia matumizi ya fedha katika hospitali na vituo vya afya nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Waganga hao uliofanyika jijini hapa.

Alisema viongozi hao ni wajibu wao kusimamia ipasavyo taratibu za fedha na kwamba matumizi ya fedha bila kupelekwa benki zikatolewa kwa taratibu za serikali yanasababisha shida.

"Hili limetuletea shida sana maana vituo vyetu vimeendelea kuwa tegemezi sana, hatuwezi kujiendesha wenyewe kwasababu fedha za cost sharing (uchangiaji huduma za afya) hazitumiki ipasavyo, hazikusanywi, hazinunulii dawa ipasavyo na kusababisha malalamiko kwa wagonjwa kuwa dawa hazitoshi," alisema.

Naibu Waziri Dugange alisema kumekuwapo na hoja nyingi za kutopeleka fedha benki na badala yake zinatumika bila kufuata taratibu za fedha za serikali.

"Naagiza kila mmoja wetu kwa nafasi yake akahakikishe anaweka mpango mkakati wa kudhibiti upotevu wa mapato kuanzia kwenye ukusanyaji hadi kwenye matumizi katika vituo vyetu," alisisitiza.

Pia alisisitiza kuwa fedha zinazotumika kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba lazima sheria za ununuzi zizingatiwe.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Maghembe, aliwataka watendaji hao kuwajibika kwenye majukumu yao kabla ya kuwajibishwa.

"Tuelewe tusipoelewana hapa mtakutana na mikono ya sheria, uwazi tumeshaambiana, na wale ambao mmejiona hapa kwenye taarifa zenu mbaya rudini mkajipange, na mtu utatafutwa popote ulipo ili kujibu tuhuma zako,"alisema.

"Tukae mguu sawa tusifurahie tu fedha zinakuja watu wanakatwa tozo mnafurahia hizi fedha ni chungu kuliko shubiri ni hatari, turudi tukajipange tufanye kazi, tukasimamie miradi," aliongeza

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Tamasha la wanawake lifungue ukurasa mpya*

**WIZARA** ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, imeandaa Tamasha la Michezo la Wanawake ambalo lilianza kufanyika tangu juzi hapa jijini Dar es Salaam kwa kutanguliwa na kongamano.

Kilele cha tamasha hilo linaloshirikisha michezo nane kinatarajiwa kufanyika leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi katika ufungaji anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Lengo kuu ya tamasha hilo lilikuwa ni kutaka kufahamu sababu kuu inayowafanya wanamichezo wanawake nchini washindwe kufanya vyema zaidi na kufahamu njia ya kutatua changamoto hizo kwa sababu hakuna kinachoshindikana.

Imeelezwa na imetolewa ushuhuda kwamba wanamichezo mbalimbali wanawake kuanzia soka, mpira wa kikapu na riadha wamekuwa wakifanya vyema katika mashindano ya kimataifa wanayoshiriki licha ya kuzingirwa na changamoto mbalimbali kuanzia wakati wa maandalizi.

Changamoto namba moja iliyotajwa ambayo inachangia kukwamisha maendeleo kwa michezo na vyama vya soka vya wanawake ni kutojitangaza kama wanamichezo wanaume wanavyofanya licha ya wao kupambana kusaka matokeo chanya.

Mara kadhaa timu au wanamichezo wanawake wamekuwa wagumu au wavivu wa kutoa taarifa za kalenda za mashindano yao jambo ambalo linawaweka kwenye wakati mgumu wa kupata wadhamini wa kusaidia kuendesha mashindano yao mbalimbali.

Kupitia tamasha hilo, viongozi na wanamichezo wanawake wametakiwa kubadilika kwa kutumia vyombo vya habari kujitangaza na kwa kufanya hivyo, si tu itawavutia wadhamini kujitokeza, lakini pia itasaidia kuongeza hamasa na ushiriki wa wachezaji kutoka sehemu mbalimbali.

Inafahamika wazi wachezaji wenye vipaji wanapatikana kuanzia ngazi za chini na ili kuwapata ni lazima chipukizi hao wafahamu uwepo wa mashindano na hapo ni rahisi kuwabaini na baadaye kuendelezwa kwa ajili ya kuzitumikia klabu au kuitwa kwenye vikosi vya timu za taifa. Wanawake pia wamekumbushwa kuajiri wataalamu katika michezo wanayoicheza na kuacha kuajiri wafanyakazi kwa mazoea, kwa sababu dunia ya sasa wachezaji wanatakiwa kuongozwa na makocha wenye weledi ambao watawasaidia kukabiliana na ushindani pale watakapokwenda kuchuana kimataifa.

Wachezaji wanaopata misingi sahihi, huwa imara na tayari kuipa matokeo chanya klabu au nchi yake kila wanapokwenda kupeperusha bendera katika mashindano watakayoshiriki.

Wanawake pia wamekumbushwa kuwa katika mstari wa mbele kutumia njia za kisasa za mawasiliano ili kujitangaza na kuwavutia wadhamini kama ambavyo matakwa halisi yanavyotulazimisha kwenda na kasi hiyo.


Lakini pia wanawake wamekumbushwa kutumia vyombo vya habari katika matukio chanya, kuheshimu katiba zao lakini pia kutokaribisha migogoro baina yao na kuweka mbele maslahi ya mchezo husika.

Tukumbuke kwa sasa nchi inaongozwa na Rais mwanamke ambaye ameweka mabilioni kwa ajili ya kuendeleza michezo hapa nchini. Si kwamba anafanya hivyo kwa makosa, bali nia na malengo ya kiongozi wetu ni kuona timu za Tanzania zinakuwa vinara na washindani kwenye michuano mbalimbali wanayokwenda kushiriki.

Tunawakumbusha kufanya vizuri kwa wanamichezo wanawake, mbali na kulipa taifa sifa, pia kutasaidia kuwanyanyua kiuchumi na kuwaepusha na majanga yanayoweza kuwatokea kwa kutumia muda mwingi kufanya mazoezi.

Sifa ya kwanza ya mwanamichezo ni nidhamu, hivyo kama wanamichezo wanawake watakuwa na nidhamu, ni dhahiri jamii inayowazunguka kuanzia katika familia wanazotoka, hali itakuwa nzuri na nchi itakuwa na mabadiliko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# *Upendo kati ya ndugu*

**NIJAPOSEMA** kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi." (1Korinto 13:1-2.)

"Upendo huvumilia, hufadhili; hauhusudu, hautakabari, haujivuni, haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya. Haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote; hutumaini yote, hustahimili yote." (1Korinto 13:4-7)

Simba na Yanga hazipiki chungu kimoja kwani zinakaliana mguu- kausha kila upande ukisema vibaya kwa mwingine. Pamoja na chuki zao, eti zasemwa ni 'watani wa jadi.' Lahaula (neno linalodhihirisha mshangao au sikitiko)! 'Watani' ni mahali asilia pa mtu, atokako mtu; nchi, taifa, dola, mji.

Simba na Yanga ni timu za jiji moja liitwalo Dar es Salaam, ukipenda waweza kuliita Bandari ya Salama kama lilivyoitwa zamani. Jiji hili lipo katika nchi moja iliyoitwa Tanganyika ambayo sasa yajulikana kwa jina la Tanzania baada ya kuungana na Zanzibar. Ni jumuia ya watu wenye historia moja, utamaduni mmoja, na mfumo wa uchumi na siasa ya utawala mmoja-TANZANIA.

Kama ndivyo, kwa nini Simba na Yanga ziwekeane shonde yaani hali ya watu kutozungumza pamoja kutokana na ugomvi wao wa zamani hata zikatengana muda mfupi baada ya kuwa timu moja? Timu hizi zilizokuwa moja mwaka 1935 zilitengana mwaka 1936 na moja kujiita Sunderland hatimae ikabadili jina na kujiita Simba walipofungua jengo lao kando ya barabara ya Msimbazi.

Eti sasa timu hizo zaitwa 'watani wa jadi.' Watani wa jadi hawawezi kufanyiana ujinga na kuwekeana shonde yaani hali ya watu kutosemezana kutokana na ugomvi wao wa zamani, mfundo, chuki, uhasidi.

Kwa sababu hiyo, sasa zimekaliana arijojo, yaani hali ya kupotezana, hali ya kupoteza mwelekeo. Pia uendaji usio na mwelekeo mwafaka kwa kukosa kuongozwa au kupangiliwa vizuri. Kilichobaki kati yao ni kushambuliana kwa maneno, kupeana majina machafu kwenye vyombo vya habari mitandaoni na mitaani!

Jambo lingine la kushangaza ni timu hizo zinapocheza na timu ngeni zinazokuja humu nchini. Hushangiliwa sana zinapocheza na Simba au Yanga, hata zinapo kwenda kucheza nje ya Tanzania halafu mojawapo kushindwa! Timu ngeni zinapokuja nchini kucheza na Simba au Yanga hushangiliwa sana zinapozishinda timu hizo! Twaonyesha ubwege (upumbavu) wetu kwa timu ngeni. Twajidharau na kujicheka wenyewe!

Wahenga walikuwa sahihi kabisa waliposema: "Wajinga ndio waliwao" wakimaanisha wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Maana yake wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Leo timu za nchi moja na eneo moja la jiji moja eti zazishangilia timu za nchi za nje zinapokuja nchini kupambana na timu za Simba au Yanga kisha twazizomea timu zetu na kuchekana wenyewe kwa wenyewe! Hatujui kuwa tunajidhalilisha wenyewe? Hali hii yadhihirisha kuwa: "Wajinga ndio waliwao."

Maana yake wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii hutumiwa kumpia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana kumbe twajidhuru wenyewe!

Tanzania ina timu nne (Simba, Yanga, Azam na Biashara United) zinazoshiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), msimu huu. Hii ni nafasi nzuri kwa Tanzania kuzishinda timu za nje kama tutazishangilia timu zetu kwa bidii na upendo kwani sote ni Watanzania.

Hata wahenga walituachia methali kuwa: "Majuto ni mjukuu mwishowe huja kinyume." Kwa kawaida mtu hajuti kabla ya kutenda jambo fulani; Hujuta baadaye wakati ambapo majuto yake hayatafaa kitu kwani ameshafanya jambo lenyewe.

Methali hii yatunasihi tuyawaze mambo kabla ya kuyafanya. Tusifanye mambo ovyo pasi na kuyawazia tusije tukajuta baadaye.

**marobarnabas@yahoo.com**

# DC awaangukia wadau wa elimu

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, amewaomba wadau wa elimu kushirikiana na uongozi wa wilaya kutatua kero ya uhaba wa walimu na miundombinu katika shule za msingi na sekondari.

Meja Gowele alitoa rai hiyo jana alipokuwa akifungua kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika Utete na kujumuisha benki ya NMB na CAMFED.

Alisema wilaya inatarajiwa kuwa na ongezeko la wanafunzi wa kidato cha kwanza kutokana mfumo wa elimu bure hapa nchini, hivyo jitihada zinatakiwa katika kujenga vyumba vya madarasa na miundombinu mingine kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Mbali na ongezeko la wanafunzi, kuhitajika ujenzi wa madarasa, aliomba wadau hao kushirikiana katika kupata walimu wengi wa kujitolea hasa kwa masomo ya sayansi na hisabati, utaratibu ambao utasaidia kupunguza uhaba uliopo.

Alisema walimu hao watakaopatikana wataendelea kusaidia kufundisha masomo hayo wakati wakisubiri walimu watakaoajiriwa.

"Tunatarajia ushirikiano wenu katika kutekeleza mikakati itakayowekwa, ambayo itaondoa vikwazo vya ufaulu katika wilaya yetu," alisema.

Meja Gowele aliwataka wazazi na walezi kuendelea kuhimiza watoto kujiunga na shule kwa kuwa gharama za shule za msingi na sekondari kwa kidato cha Kwanza hadi cha nne ni bure, pia wasimamie mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Juma Ligomba, aliwataka viongozi wa wilaya hiyo, kusimamia na kuhakikisha wanafunzi watakaochaguliwa wanajiunga na kidato cha kwanza na wenye umri wa kuanza shule ya msingi wanafanya hivyo.

Akitoa taarifa ya elimu kwa shule za msingi, Kaimu Ofisa Elimu Msingi, Fatuma Kimolo, alisema idara hiyo inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 294 kulingalinisha na mahitaji, ambayo ni madarasa 716.

Kwa upande wa matundu ya vyoo, alisema yaliyopo ni 504, huku mahitaji yakiwa 1,530 na madawati yanayohitajika ni 10,843 wakati yaliyopo ni 8,690.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, akionyesha kondom aina ya safari inayosambazwa na shirika la vijana nchini (TAYOA), kwenye maonyesho yaliyofanyika pembeni ya mkutano wa waganga wakuu wa mikoa na halmashauri, jijini Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Bosi CRDB apenya orodha watendaji bora 50 Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Utafiti ya Reputation Poll International LLC, imemtaja Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, kuwa miongoni mwa watendaji wakuu 50 wenye sifa nzuri kiutendaji barani Afrika kwa mwaka huu.

Nsekela amefanikiwa kuwa mmoja wa watendaji wakuu wa benki barani Afrika walioonyesha weledi katika sekta ya uwekezaji na uvumbuzi wa kiteknolojia katika kipindi hicho ambacho dunia inapambana na janga la corona.

Kampuni hiyo imesema iliona umuhimu wa kuwatambua viongozi katika sekta ya benki kwa kutambua mchango wa sekta hiyo katika jamii, kuunganisha watu na biashara pamoja na uchumi kiujumla kwa njia moja au nyingine.

Utafiti huo unaofanywa kila mwaka, uliangalia pia mchango wa watendaji wakuu wa benki 50 barani Afrika namna waliochochea au kupitia nafasi zao kufanya mapinduzi ya kisekta katika maeneo ya ubora, uadilifu, uaminifu, utaalamu, teknolojia na urahisi wa upatikanaji wa mikopo.

Katika orodha yao, jina la Nsekela lilikua la kwanza katika orodha ya watendaji wakuu Afrika na ni Mtanzania pekee aliyeorodheshwa na kampuni hiyo.

Hata hivyo, hii ni mara ya pili kwa Nsekela kutambulika kimataifa kupitia uongozi wake baada ya mwaka jana kutajwa katika jukwaa la viongozi bora na Jarida la African Leadership Magazine.

Taarifa ya kampuni hiyo ilisema tasnia ya benki iliathirika kwa kiasi kikubwa na corona hasa kwa nchi za Afrika na kusababisha faida kwenye mitaji kupungua hadi kufikia asilimia saba mwaka 2020 kutoka asilimia 14 mwaka 2019 (McKinsley, 2021).

Hata hivyo, chini ya Nsekela, CRDB iliendelea kutengeneza faida mwaka hadi mwaka.

Tangu alipojiunga na benki hii mwaka 2018 kama Mtendaji Mkuu, Benki ya CRDB imekuwa ikiwekeza kwa kiasi kikubwa katika mifumo ya kidijitali, ikiwa ni moja ya vitu vilivyochangia ukuaji wa faida kwa zaidi ya asilimia 87 mwaka 2019 na kufikia Sh. bilioni 120 kutoka Sh. bilioni 64.2 zilizopatikana kama faida mwaka 2018.

Katika miaka yake mitatu ndani ya benki hiyo, utendaji wa CRDB umeimarika ukichochewa na mageuzi ya kimkakati.

Mwaka jana benki hiyo ilivunja rekodi kwa kuongeza faida yake kwa asilimia 35 na kufikia Sh. bilioni 236 kutoka Sh. bilioni 175 za mwaka 2019.

Taarifa hiyo ilisema katika matokeo ya fedha ya nusu ya mwaka huu, benki iliweza kuongeza faida yake kwa asilimia 26 kufikia Sh. bilioni 88.6 kulinganisha na Sh. bilioni 70.4 zilizopatikana nusu ya mwaka jana.

Nsekela alisema ni jambo jema kuwa miongoni mwa viongozi wenye utendaji bora Afrika na mafanikio hayo yamechangiwa na wateja, wadau na wafanyakazi wa benki hiyo.

Alisema licha ya matatizo ya corona, CRDB imeendelea kupata matokeo mazuri ya kifedha kutokana na ukuaji mzuri wa mapato na faida. Alisema uwekezaji thabiti katika mifumo ya kidijitali umewezesha zaidi ya asilimia 80 ya miamala kufanywa nje ya matawi ya benki na kuongeza ujumuishaji kifedha kulingana na ajenda ya serikali.

"Tumeongeza kasi ya miradi ya kujipambanua kidijitali ili kuhakikisha kuwa tunahudumia wateja wetu kwa ufanisi wakati pia tukizingatia miongozo ya afya.

"Lengo ni kuendesha matumizi ya njia za dijitali kama SimBanking, Internet banking na CRDB Wakala, ambazo itapunguza umuhimu wa wateja wetu kutembelea matawi," alisema.

# Watumishi 7 halmashauri wafukuzwa kazi

**Na Richard Makore,** MISUNGWI

WATUMISHI saba katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, wamefukuzwa kazi na wengine wanne kupewa onyo kwa makosa mbalimbali.

Hayo yalibainishwa juzi katika kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika katika halmashauri hiyo baada ya kujiridhisha na uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili watumishi hao.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Kashinje Erasto, aliwataja watumishi hao kuwa ni watendaji wa vijiji vinne, mtendaji wa kata, madereva wawili, mlinzi, madaktari wawili na mkaguzi msaidizi wa zahanati. "Tunaendelea kusisitiza kwamba tutaendelea kuzingatia misingi ya kisheria katika kuhakikisha tunatoa haki kwa watumishi," alisema Kashinje. Aidha, mwenyekiti huyo alisema zahanati nyingi zilizojengwa kwa nguvu za wananchi hazijafunguliwa kwa sababu hazina watumishi.

Alisema bado wanakabiliwa na uhaba wa zaidi ya watumishi 1,000 katika sekta mbalimbali hasa afya na elimu.

Kutokana na uhaba huo, aliiomba serikali kuliona hilo kwa kufungua mianya ya kutosha na kutoa ajira kwa watumishi katika sekta hizo. Naye Diwani wa Sumbugu, Jogoli Kasatu, aliwataka watumishi kuzingatia taratibu na sheria za utumishi kwa kuwa hawatasita kuwachukulia hatua watakaoenda kinyume na taratibu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Leokadia Humera, alisema halmashauri bado inakabiliwa na uhaba wa watumishi huku akisema ufinyu wa mapato ya ndani unasababisha kukwama kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema wanaendelea kuwahamasisha wananchi kuiweka wilaya hiyo katika mazingira mazuri kwa manufaa ya umma.

"Tunaendelea kuwahamasisha wananchi na wadau wengine kuweka Wilaya ya Misungwi katika mazingira ya amani, utulivu, ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za maendeleo na utunzaji wa rasilimali za umma kwa manufaa ya umma," alisema Humera.

# Waziri aona shida utoaji wa vibali vya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande, amezitaka mamlaka zinazohusika katika utoaji wa vibali vya uwekezaji kuwashirikisha maofisa mazingira kutoka serikali za mitaa ili kuepusha migogoro na vikwazo mbalimbali.

Chande alitoa wito huo jana alipozungumza katika kikao kazi na maofisa mazingira kutoka Halmashauri ya Mji wa Babati na Wilaya ya Babati alipozuru kikazi mkoani Manyara. Alisema maofisa mazingira wamekuwa hawashirikishwi kikamilifu katika michakato ya kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya biashara, hatua inayowafanya washindwe kutambua wajibu wao.

"Kuna mtu alinunua eneo kwa ajili ya makazi lakini kinyume chake akabadilisha matumizi na kulifanya kituo cha mafuta na iligundulika kuwa kumbe maofisa mazingira wala halmashauri zao hawakushirikishwa.

"Katika maendeleo ubora ya maisha ya mwanadamu ni uwapo wa mazingira kwa sababu mazingira ndio uhai wetu, ndio sehemu ya maisha yetu, hivyo ni lazima tuweke mkazo katika utunzaji wa mazingira, pia pamoja na kujali uchumi wetu tusisahau suala zima la utunzaji wa mazingira," alisema.

Naibu Waziri Chande alitahadharisha kuhusu athari za kelele kuwa za kiwango kikubwa kutokana na ukuaji wa miji na ambayo husababishwa na uwapo wa fursa kwa wananchi akisema kuwa si jambo baya lakini uwekezaji usikwaze watu wengine.

"Uwekezaji ni mzuri lakini je, unawekeza kwa misingi gani na uwekezaji wako hauwakwazi wengine wanaokuzunguka?

"Hatuwezi kukuangalia wewe mmoja kwa maslahi yako ukawa unaangamiza ama unateketeza wananchi walio wengi," alisema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Chande ametembelea Kiwanda cha Sukari Manyara kilichoko wilayani Babati, akiwapongeza kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira pamoja na kutengeneza mkaa mbadala kutokana na makapi ya miwa.

Alitoa wito kwa uongozi wa kiwanda hicho kusambaza nishati hiyo mbadala inayozalishwa kiwandani hapo kwa wananchi na kwa bei nafuu ili kusaidia kupunguza ukataji holela wa miti.

Hata hivyo, Meneja Kanda wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Lewis Nzali, pamoja na pongezi kwa kiwanda hicho, alibainisha baadhi ya vikwazo vikiwamo ukosefu wa vifaa kinga kwa wafanyakazi na wageni wanaotembelea, hali inayoweza kusababisha athari za kiafya.

Alionyesha wasiwasi kutokana na mvuke wenye joto kali unaotoka wakati wafanyakazi hao wakiwa kazini ambapo alishauri itafutwe namna bora ya kupunguza muda wa kukaa katika joto.

Pia alishauri kiwanda kiajiri mtaalamu wa mazingira na usalama katika kiwanda ili kuwashauri nini cha kufanya ili kulinda mazingira na usalama wa wafanyakazi kwa ujumla.

Awali akitoa taarifa, Ofisa Uhusiano wa Kiwanda hicho, John Geu, alisema kwa vile miwa hutumia maji mengi katika uzalishaji wanatumia maji ya visima badala ya mto ambao ni chanzo kikuu cha maji.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wanalinda na kuhifadhi mazingira wamepanda miti pembezoni mwa mto.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande (wapili kushoto), akiwa katika ziara kwenye kiwanda cha sukari cha Manyara wilayani Babati juzi. **PICHA: OMR**

# Mbunge aomba nguvu kwa DC kutatua kero bodaboda

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amemwomba Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, washirikiane kutatua kero ya waendesha daladala, bajaji, pikipiki na wafanyabiashara wadogo wanaopaswa kutengewa maeneo rafiki kwa ajili ya kufanya shughuli zao.

Abood alitoa rai hiyo kwa kiongozi huyo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika eneo la stendi ya zamani ya daladala na kukutanisha makundi hayo kwa ajili ya kusikiliza kero zao ili kuzipatia ufumbuzi wa pamoja.

Mbunge huyo akizungumza katika mkutano huo, alisema amekuwa akipokea kero za muda mrefu kutoka kwa makundi hayo ikiwamo kero za vituo vya daladala, bajaji na bodaboda vilivyotengwa sio rafiki katika utoaji wa huduma za usafiri.

Alisema katika malalamiko ya makundi hayo, wamekuwa wakisisitiza kuwa ili kutatua kero hizo, wameomba Manispaa irudishe stendi ya zamani ya daladala iliyoko katikati ya mji, hatua ambayo itasaidia kupunguza msongamano na ajali.

"Mkuu wa Wilaya kwanza nikupongeze kwa ufafanuzi wa machinga maana kulikuwa na malalamiko mengi, ninadhani watu wameshaelewa.

"Sasa nimalizie tu kwa kuwa wewe una mamlaka katika wilaya hii, hili suala la kurudi stendi ya daladala hapa mjini ninaomba tushirikiane ili stendi irudi hapa," alisema.

Akizungumza katika mkutano huo, Msando alisema tayari alishapokea malalamiko ya makundi hayo katika ofisi yake na alishauri Baraza la Madiwani liketi na kupitia upya uamuzi wa kuhamisha stendi hiyo kwenda Mafiga kwa kuwa malengo hayajaleta tija kutokana na mapato yake kuwa madogo.

Kiongozi huyo pia alishauri halmashauri, Kikosi cha Usalama Barabarani na Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu (LATRA) kukaa kwa pamoja kupanga utaratibu wa stendi ya Mafiga iweze kutumika kwa mabasi yanayofanya safari nje ya Manispaa ya Morogoro kwa kuweka tozo ambayo haitolalamikiwa na wasafirishaji.

Akizungumzia kuhusu vituo vya kupakia na kushusha abiria vya bajaji na bodaboda, Msando aliagiza Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na Manispaa kupitia upya vituo na kuviongeza ili kuwa rafiki kwa watumiaji.

Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kianga, akizungumzia kuhusu ombi la waendesha daladala kurudishiwa stendi ya zamani, alisema kwa vile uamuzi huo ulifanywa na Baraza la Madiwani, ombi hilo ataliwasilisha kwenye kikao cha baraza hilo ili lijadiliwe na kupatiwa uamuzi mwingine.

Awali akiwasilisha malalamiko yao, Rajabu Msofo, ambaye ni dereva wa bodaboda, aliunga mkono kurudishwa kwa stendi hiyo ya zamani kwa kuwa ilikuwa ikiwanufaisha waendesha bodaboda kupata abiria pale abiria wanapofikia mwisho wa safari yao tofauti na sasa hivi ambapo abiria hawana kituo maalum.

# Vodacom yaja na 'Dunia Kijiji'

**Na Romana Mallya**

VODACOM Tanzania Plc imezindua awamu ya pili ya mpango wake wa upanuzi wa huduma za malipo ya kimataifa kupitia kampeni mpya iitwayo 'Dunia Kijiji, Afrika Mashariki ni Yako'

Akizungumza juzi mkoani Dar es Salaam katika uzinduzi huo, Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema kupitia kampeni hiyo sasa malipo ya moja kwa moja yanawezekana kutoka M-Pesa kwenda benki zote katika nchi za Afrika Mashariki ambazo ni Burundi, Kenya, Uganda na Rwanda.

Alisema Vodacom ndiyo kampuni ya kwanza kuanzisha huduma za kifedha kwa mtandao na imejenga msingi imara wa kuendeleza upatikanaji wa huduma hizo kama vile malipo ya bili, akiba, mikopo pamoja na malipo ya biashara.

"Kwa sasa tunakuwezesha kutuma fedha kwenda benki mbalimbali Afrika Mashariki, tunaamini huduma hii itawaondolea usumbufu wateja ambao walikuwa wanatembea na fedha.

"Kwa sasa mambo muhimu kama mahitaji ya kifamilia, miamala ya kibiashara au gharama za shule mteja atatuma kwa urahisi na tumejiunganisha na benki zaidi 60 za Afrika Mashariki," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa M-Pesa inawahudumia wateja 240,000 kwa mwezi wanaopokea fedha kimataifa.

Mkurugenzi wa Terrapay wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Willie Kanyeki, alisema huduma hiyo itawarahisishia wateja kufanya malipo ya fedha kimataifa.

Meneja Kitengo cha Diaspora wa Benki ya Equity, Doreen Raphael, ambao ni washirika wa Vodacom, alisema wanafurahi kuendelea kushirikiana nao katika kuwezesha malipo kwa gharama nafuu zaidi na kwa urahisi.





# Waziri asema kasi wizi mtandaoni inatisha

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema miamala iliyoko hatarini kwa wizi wa mitandaoni ni kati ya Sh. milioni 500 na Sh. bilioni moja kwa siku.

Aidha, ameagiza vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini kuwatafuta watu wote wanaowachafua wenzao mitandaoni hasa wale wanaomdhihaki Rais Samia Suluhu Hassan.

"Wizi wa mitandaoni ni mkubwa sana. Kwa siku takribani Sh. milioni 500 hadi Sh. bilioni moja zinakuwa kwenye 'transactions' (miamala) za (ya) wizi. Hii ni hatari kwa uchumi wa nchi na kesi za namna hii zinaweza kuhesabu kwamba ni uhujumu uchumi," alisema Simbachawene alipozungumza na waandishi wa habari jana.

Simbachawene alisema wizi wa namna hiyo haukubaliki kwa kuwa unarudisha nyuma maendeleo ya watu, hivyo kulitaka Jeshi la Polisi kuanza msako mkali ili kuwabaini wahalifu hao ambao wanasumbua jamii.

"Hii mitandao itumike kwa kazi zenye manufaa na si kwa wizi wa mitandao na kuwarudisha nyuma watu wenye malengo ya kuinukakiuchumi," alisema Simbachawene.

Alisema wizi wa mitandaoni umekuwa hatari kubwa sana kwa sababu fedha hizo ni nyingi na suala hilo halipaswi kufumbiwa macho hata kidogo.

Simbachawene alisema wizi wa aina hiyo baada ya muda mfupi utakuwa ni historia na watahakikisha kesi zote zinaorodheshwa na kuwekwa kwenye kanzidata ya wizi wa kimtandao.

Alisema wastaafu wanakuta fedha zote za mafao zimeondolewa na kutaka jeshi la polisi liamke na kuwasaka watu wa aina hiyo ikiwamo kesi za aina hiyo zifanyiwe kazi kwa haraka.

Kuhusu matusi mitandaoni, alisema watu wameachiwa uhuru sana wa mitandaoni, hivyo kila mtu ana haki ya kutumia mtandao lakini asiutumie kwa kutukana watumitandaoni badala ya kufanya kazi ya msingi.

Aliwaonya askari wanaowadai raia fedha ili kufuatilia wizi wa vitu vyao na kuagiza hao wanapaswa kuchukuliwa hatua kama wahalifu wengine.

Simbachawene alisema jamii inapaswa kutoa taarifa kwa viongozi wa juu ili kuhakikisha askari wa aina hiyo wanakamatwa kwa sababu wanaliaibisha jeshi hilo.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli, akizungumza wakati akifunga mkutano wa tatu wa walimu wakuu wa shule za msingi nchini, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mkumbo ataka uhuru wa kisera nchi zinazoendelea

**Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ya Tanzania imetaka kuwapo na uhuru wa kisera kwa nchi zinazoendelea na maskini ili kujihami na athari za uingizwaji uliokithiri wa bidhaa za kilimo hususan kutoka nchi zilizoendelea.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof.Kitila Mkumbo, alisema hayo jana katika Mkutano wa Mawaziri wa Kundi la Nchi 33 (G33) wanachama wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) uliofanyika kwa njia ya mtandao. Prof. Mkumbo aliongoza ujumbe kutoka Tanzania.

Kundi hilo linajumuisha nchi wanachama zenye maslahi yanayofanana ya kutaka uwazi na manufaa katika majadiliano ya WTO yanayohusu kilimo. Lengo la mkutano ni kujadili na kuweka msimamo wa pamoja katika maeneo ya kipaumbele kwenye kilimo.

Prof. Mkumbo alibainisha msimamo wa Tanzania kwenye maeneo mbalimbali ambao unaungwa mkono na nchi zingine wanachama kwenye eneo la misaada ya upendeleo.

"Msimamo wa Tanzania ni kuwa na makubaliano ya WTO yanayokataza na kuweka vikwazo kwa nchi zilizoendelea wanachama wa shirika hilo kutoa misaada kwa wazalishaji wao inayoathiri biashara za nchi zingine wanachama. Hii ni pamoja na kutaka uwapo uwazi kwa nchi zilizoendelea kwa mfano katika utoaji ruzuku kwa wakulima wao," alisema.

Pia alisema Tanzania imesisitiza kutaka nchi zinazoendelea na maskini wanachama wa WTO kuwa na uhuru wa kuhifadhi chakula kwa madhumuni ya usalama wa chakula.

Mkutano huo umeongozwa na Mwenyekiti Mhe. Muammad Lutfi, Waziri wa Indonesia anayesimamia biashara ambapo ulihudhuriwa pia na Mkurugenzi Mtendaji wa WTO Ngozi Okonjo-Iweala na ulikuwa sehemu ya maandalizi ya nchi hizo katika mkutano wa 12 wa ngazi ya juu wa maamuzi wa WTO (MC12) unaotarajiwa kufanyika mjini Geneva, Uswisi Desemba, mwaka huu.

## Watakiwa kutumia mawasiliano kiofisi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WALIMU wakuu wa shule za msingi nchini wametakiwa kutumia njia sahihi za mawasiliano ya kiofisi na vikao ili kusaidia kuondoa malalamiko ya walimu kwenye maeneo yao ya kazi.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mkutano mkuu wa tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu Tanzania Bara (TAPSHA).

"Unakuta kuna mwalimu anaandika barua ya kutaka kuhama au ana malalamiko wewe unaikalia barua hiyo bila kuijibu au kushauri njia sahihi. Nawataka mkashughulikie kero ndogo ndogo huko kwenye maeneo yenu," alisema.

Pia aliwataka kuwasikiliza malalamiko yao wale wanao waongoza kwa sababu wao ni maofisa katika ngazi hizo za shule wanazozisimamia.

Alibanisha kuwa kazi ya kiongozi ni kusimamia na kuongoza wale walio chini yao akishindwa huyo hafai kuwa kiongozi kwa sababu inasababisha migomo isiyo na tija .

Mweli pia aliwashauri wakuu hao kuwashirikisha wazazi na halmashauri katika suala la chakula shuleni kwa sababu kuna wanafunzi wanashindwa kufanya vizuri kwenye masomo kwa sababu ya njaa.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa wanafunzi wanaopata lishe shuleni uwezo wao wa kimasomo na mahudhurio shuleni ni mazuri kwa sababu wanakuwa na nguvu ya kimwili.

"Kuna shule zipo mbali mwanafunzi anafika shuleni amechoka na shule haina utaratibu wa chakula kwa kweli hiyo ni kuwaumiza watoto wetu, naomba mkakae na wazazi ili kuangalia utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi kupata chakula shuleni," alisema.

Mwenyekiti wa TAPSHA, Rehema Remole, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2019 kwa lengo la kuwakutanisha walimu hao ili kubadilishana uzoefu wa kitaaluma.

Alisema katika mkutano huo kulikuwa na mada mbalimbali zilizotolewa na TAMISEMI, vyuo vya ualimu na wengine kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa lengo la kujengewa uwezo wa kazi.



# Maandalizi ya ujenzi wa barabara yakamilika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema maandalizi ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 22.1 ya Chakechake hadi Wete kisiwani Pemba yameanza ikiwa ni kuelekea malengo ya kukifanya kisiwa hicho kuwa ukanda maalumu wa uwekezaji katika Afrika Mashariki.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Rahma Kassim Ali, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu ujenzi wa barabara hiyo ambayo imekwama kwa muda mrefu baada ya kujitokeza kwa kasoro mbalimbali.

Alisema tayari imepatikana kampuni itakayofanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa barabara hiyo ambayo ni muhimu kwa kukiunganisha kisiwa cha Pemba na mikoa miwili.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete iko katika hatua za mwisho za kufanyiwa upembuzi yakinifu na ujenzi wake baada ya kupatikana kampuni itakayofanya kazi hiyo," alisema.

Waziri huyo alisema ujenzi wa barabara hiyo unakamilisha ndoto ya kuyafikia malengo ya kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa ukanda maalumu wa uwekezaji kiuchumi.

Alisema miongoni mwa maeneo yatakayofaidika na ujenzi wa barabara hiyo ni maeneo huru ya uchumi yaliyoko Micheweni.

"Ujenzi wa barabara hiyo utafunguwa fursa za kiuchumi kwa wawekezaji kuwekeza katika maeneo huru ya uchumi na uwekezaji huko Micheweni. Miongoni mwa vikwazo katika uwekezaji ni miundombinu mibovu," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Muhammed, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Spika awa mbogo mahudhurio hafifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amewataka Wawakilishi kutekeleza kanuni za baraza hilo ambazo zinasisitisa suala la mahudhurio ya vikao pamoja na kamati za baraza.

Spika Zubeir aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa za baraza kwa wajumbe na kusema Mwakilishi wa Chwaka kwa tiketi ya CCM, Issa Haji Ussi, amekuwa na tabia ya kushindwa kuhudhuria vikao vya Baraza la Wawakilishi pamoja na kamati bila taarifa za ofisi. Kwa mfano amesema mwakilishi huyo hajahudhuria vikao vya kamati yake ya bajeti kwa wiki tatu bila taarifa kutoka kwa ofisi ya Spika au mwenyekiti wa kamati.

Aidha, alisema hata mkutano wa Baraza la Wawakilishi unaoendelea sasa mwakilishi huyo hajahudhuria vikao bila taarifa kwa Spika.

Spika alisema suala la kuhudhuria vikao vya Baraza la Bawakilishi linaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za kudumu za baraza toleo la mwaka 2020 pamoja na kanuni ya 75.

"Mjumbe yoyote atakayekosa kuhudhuria vikao vya baraza au kamati visivyopunguwa vitano mfululizo bila ya kutoa taarifa kwa Spika au mwenyekiti wa kamati za baraza basi basi mjumbe huyo atatangazwa na Spika kuwa na tabia ya utoro," alisema.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni hiyo suala hilo Spika atalazimika kuwasilisha taarifa hizo kwa chama anachotokea mjumbe huyo kwa hatua zaidi.

"Waheshimiwa wajumbe kwa kuwa mwakilishi Issa Haji Ussi hakuhudhuria kazi za kamati na shughuli za baraza la wawakilishi kwa kipindi chote hicho kinyume na kanuni ya 75 namtangaza rasmi mwakilishi huyo kuwa ana tabia ya utoro"amesema.

Ussi, maarufu kama Gavu, ni mwakilishi wa jimbo la Chwaka kwa tiketi ya CCM vipindi viwili sasa. Kipindi kilichopita alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu.

# Wakala Usajili Matukio kupatiwa vitendea kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika mwaka wa fedha 2021/22, kipaumbele chake ni kuipatia taasisi hiyo vitendea kazi kwa ajili ya kuleta ufanisi wa majukumu yake.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu (SMZ), Masoud Ali Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtambile, Mohamed Mgaza Jecha, aliyetaka kujua mikakati ya serikali ya kuimarisha taasisi hiyo.

Mohamed alisema Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imeanzishwa kwa ajili ya kurahisisha mambo muhimu ya msingi yanayohusu jamii ikiwamo upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi pamoja na vyeti vya kuzaliwa.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu hayo, serikali inakusudia kuwapatia vitendea kazi wafanyakazi wa wakala wa usajili wa matukio ya kijamii kwa ajili ya kuzifikia shehia mbalimbali na kukamilisha usajili huo.


Waziri alisema vitendea kazi hivyo yakiwamo magari na emo gari na vipande vyengine kwa ajili ya kuwafikia wananchi na kutekeleza majukumu ya kufanya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi pamoja na vyeti vya kuzaliwa.

Aliwataka wananchi kujitokeza kukamilisha usajili wa matukio ya kijamii na kuongeza kuwa upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi ni haki ya kisheria kwa kila mwananchi aliyefika umri wa miaka 18.

"Hakuna vikwazo wala ubaguzi katika upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi na ni haki kwa kila mwananchi mwenye sifa. Kitambulisho hicho hutumika kwa ajili ya shughuli muhimu za kijamii," alisema.

"Mheshimiwa Mwenyekiti napenda niwajulishe wananchi wajitokeze kwa wingi kufanya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi pamoja na vyeti vya kuzaliwa ili kuondosha usumbufu unaoweza kujitokeza,' alisisitiza.

**Waziri alisema vitendea kazi hivyo yakiwamo magari na emo gari na vipande vyengine kwa ajili ya kuwafikia wananchi na kutekeleza majukumu ya kufanya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi pamoja na vyeti vya kuzaliwa.**



**RAPCHA**

UKURASA 12






# KAMA KWELI Wema Sepetu kajiepusha na mengi

WATU wengi wanahoji mwonekano mpya wa nyota wa filamu nchini Wema Sepetu, wakiamini msanii huyo amefanya upasuaji maalum wa kupunguza uzito.

Hofu ya watu hao ni kuona nini kitakachotokea kama Wema, amechukua hatua hiyo ngumu na yenye gharama kubwa. Pamoja na mwigizaji huyo kuwa na umbo jembamba linalokaa vyema kila nguo anazovaa, lakini haijafahamika kama umbo hilo litadumu au kuna siku atarejea kama zamani.

Hata hivyo, kitaalam inaonyesha kwamba upasuaji wa kupoteza uzito au upasuaji wa bariatric una faida kubwa kiafya, hasa katika kujilinda na magonjwa ya saratani, moyo na kiharusi.

Aina hii ya upasuaji sio njia ya mkato wa kupoteza uzito au kuhusu kupata mwili unaovutia. Upasuaji wa Bariatric hufanyika tu kwa lengo kuu kuzuia matatizo ya afya.

Mtu akizidiwa na uzito ni rahisi kupata magonjwa ya kisukari, ugonjwa wa moyo, HYPERLINK "https://sw.approby.com/miongozo-ya-malengo-ya-shinikizo-la-damu/" shinikizo la damu , na HYPERLINK "https://sw.approby.com/kuwa-overweight-mara-mbili-nafasi-yako-ya-kuwa-na-kiharusi/" kiharusi .

Hata hivyo, haipendekezwi kufanyika upasuaji wa bariatric, kwa ajili ya urembo ni lazima daktari apendekeze kwamba una sababu za msingi.

Kuna aina nyingi ya upasuaji wa kupoteza uzito, mfano bypass ambayo upunguza tumbo, ambapo chakula ambacho mtu hula huingia ndani ya tumbo kidogo baada ya kuingia kingi.

Aina nyingine za kawaida za upasuaji wa bariatric ni 'banding' ya tumbo. Hapa inahusisha upasuaji kuweka kifaa bandia kwenye tumbo, ili kujenga hisia ya ukamilifu .

Njia zote hizi ni njia nzuri ya kuzuia kalori na husababisha kupoteza uzito na kuzuia uzito.

**Kwa msaada wa mtandao**



# Eucharia umewagundua wapenda sifa

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Eucharia Anunobi, amewaponda baadhi ya watu wanaotumia kiki za ajabu kwa ajili ya kupata umaarufu katika mitandao ya kijamii.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Eucharia, amesema watu wa aina hiyo wanatumia harusi hewa na mambo yao binafsi kwa kuyaweka katika mitandao ya kijamii.

"Umeshuhudia watu wapo tayari kuweka mambo yao kama harusi hewa, uhusiano wa kimapenzi na mambo binafsi wakitaka kuwa maarufu kwenye mitandao ya kijamii," amesema.



## Britney kufuta si kuwakimbia watu

MWANAMUZIKI wa Marekani, Britney Spears, ameamua kujitenga na mashabiki wake baada ya kufuta ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram.

Kulingana na mtandao wa PageSix, staa huyo wa muziki wa Pop, amechukua hatua hiyo siku chache baada ya kuvishwa pete ya uchumba na mpenzi wake wa siku nyingi Sam Asghari.

"Anajisikia furaha kwa kuwa sehemu sahihi, kuwa kimya kunaweza kuwa na nguvu na ujumbe wenye nguvu zaidi," kilisema chanzo.

## Kanye West hujui kama kakuzalia wana?

TUKIO lilowaacha midomo wazi mashabiki wa muziki duniani ni lile la rapa mkali kutoka Marekani, Kanye West, kumfuta mke wake Kim Kardashian, katika ukurasa wake wa Instagram.

Mwanamuziki huyo billionea alichukua hatua hiyo siku ya Jumatatu ya Septemba 13, ikiashiria mambo bado magumu kwa mastaa hao wawili, ambao wanaburuzana mahakamani wakidaiana talaka.

Hatua hiyo inakuja miezi michache baada ya Kanye kuwafuta wanafamilia wa kardashian katika akaunti ake ya Twitter.

Kulingana na PageSix, vyanzo mbalimbali vinasema yote yanajiri baada ya mwanamuziki huyo kudaiwa kutoka kimapenzi, nje ya ndoa na moja ya wimbo wake katika Albam yake mpya, ukieleza jinsi alivyokuwa akitoka na kumuacha mke wake ndani.





## J Lo, Ben mapenzi ya uzeeni yananoga

MWIGIZAJI mkongwe, Ben Affleck na mwanamuziki Jennifer Lopez, wameambatana kwa mara ya kwanza katika zulia jekundu wakiwa kama wapenzi.

Wawili hao wameonekana wakipigwa picha wakiwa katika hali ya mahaba wakati wa tamasha la filamu la Vanice, nchini Italia, lilofanyika siku ya Ijumaa iliyopita.

Lopez na Affleck, wamerudisha penzi lao hivi karibuni baada ya kuachana na kusababisha watu wengi kuwafuatilia kila siku kujua wanachofanya.

## Wendy achunguzwa matatizo ya akili

MWENDESHAJI wa kipindi maarufu cha mazungumzo cha televisheni, Wendy Williams, amefikishwa katika hospitali moja kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa tatizo la akili.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Wendy ambaye anajulikana sana Marekani kutokana na shoo yake hiyo, aliwahishwa na gari la wagonjwa siku ya Jumatano, baada ya kupata simu ikiomba msaada kutoka kwa mwanamke anayeishi na mtangazaji huyo.

Chanzo kimoja kinasema Wendy ambaye alipanga kurudi katika shoo yake, anakabiliwa na upweke pamoja na matatizo ya kiafya yanayomuandama.



MAKALA

# Corona ilivyoumiza soko kimataifa la wachonga vinyago wa Mwenge

## ●Baadhi wafunga virago, waihama fani



**Ally Mlanzi na Donald Lukele,**

TUDARCo

TANZANIA ni nchi iliyobarikiwa na kuwa na vivutio vingi ambayo huwavutia wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani kuja kuviangalia.

Baadhi ya vivutia hivyo ni visiwa, fukwe za bahari, milima, mbuga za wanyama na mito inayotiririsha maji kipindi chote cha mwaka.

Hata hivyo, sanaa ya uchongaji imeonekana kuwavutia sana watalii wanakuja nchini, hivyo imekuwa sekta muhimu inayowaingizia kipato wachongaji, wauzaji na taifa kwa ujumla.

Tamaduni za uchongaji wa vinyago na sanaa ya kale ambayo inapendwa na watu wengi.

Hata hivyo, biashara ya vinyago katika soko la kimataifa la Mwenge, imeshuka kwa kasi kutokana na janga la Corona na kusababisha maisha kuwa magumu kwa watu wanaojishughulisha na kazi hiyo.

Wadau wa biashara hiyo, wanasema tangu kuibuka kwa Uviko-19, kila kitu kimekwenda kombo kutokana na kushuka kwa idadi ya watalii wanaotembelea soko hilo.

Ahmad Abdallah (42) ambaye amejiajiri kupitia shughuli za uchongaji wa vinyago kwa miaka 20, anasema kipato chake kimeshuka maradufu kiasi ambacho anashindwa kuihudumia familia yake.

Abdallah mwenye mke na watoto wa wawili, anasema awali kazi hiyo ilikuwa msaada mkubwa kwake kwani ilimuingizia kipato na kufanya maendeleo mengi ikiwa kujenga nyumba na kusomesha watotowake.

“Kazi hii imenifanya nimiliki nyumba yangu na kuendesha familia yangu ingawa watu wanaweza kuona ni kazi ya kawaida,” anasema Abdallah.

Anasema kabla ya kuingia kwa corona, alikuwa akiingiza pesa nyingi kwa kuuza kinyago kimoja pekee. Hata hivyo anasema nado anachapa kazi na kufanikiwa kupata kipato cha kujikimu kimaisha.

Abdallah ambaye amejikita katika fani hii baada ya kutambua kipaji chake na kuchangamkia fursa ya kujifunza uchongaji.

Anasema vijana wa sasa wanashindwa kupata ajira kwa kushindwa kufahamu vipaji vyao na hivyo kuishia kurandaranda mitaani.

Anaeleza wengi wanataka kazi za kuajiriwa baada ya kuhitimu elimu zao, kitu ambacho si kizuri na kinawachelewesha.

**YALIYOWAKUTA KAZINI**

Abdallah anakiri kwamba kuna changamoto nyingi katika biashara hiyo, hasa baada ya kuingia kwa ugonjwa wa corona.

Anasema wateja wengi wa bidhaa zao ni wageni kutoka Ulaya, Marekani na Asia, lakini kutokana na kusambaa kwa ugonjwa huo wamepungua kuja nchini na kusababisha kushuka kwa mauzo.

Abdallah ameongeza kwa kusema Watanzania wengi hawana utamaduni wa kununua picha zilizo chorwa hata vinyago kwaajiri ya mapambo, hii inapelekea kupata hali ngumu katika mauzo.

“Maduka mengi yamefungwa na hata wafanya biashara wa kazi hizi waliamua kuacha sababu ya kushuka kwa biashara. Hata malighafi tunazotumia zimepanda bei kwasasa na hazipatikani kwa urahisi hii imekuwa ni changamoto inayotumaliza kibiashara” Anasema Abdallah

Msanii mwingine Juma Athuman(27) anaejishughulisha na uchoraji anasema tangu janga la corona limeingia ameshuhudia wenzake wakiachana na fani hii baada ya kushindwa kuendesha maisha yao.

Ameongeza kwamba kupitia fani hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa vijana wengi waliyo na ujuzi wa Sanaa kumudu kuendesha maisha yao, hata hivyo kwa sasa ni sawa na hakuna kitu.

Katibu wa Chama cha Wasanii Wachongoji Tanzania (CHAWASAWATA) Aloyce Ngwikwi(56) anasema uongozi wake umekutana na wanachama kuzungumzia suala hilo kupitia vikao mbalimbali.

Anasema kila mara wanapeleka maoni yao Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ikiwemo kutoa nafasi za maonesho kwenye bidhaa zao hasa Sabasaba.

Pia ameomba serikali kuandaa semina kwa ajili ya kuelimisha wasanii na kusaidia kupata masoko nje ya Tanzania.

Anaongeza kuwa ana imani na biashara hiyo kuwa nzuri muda mfupi ujao, kwani viashiria vinaonyesha imeanza kurejea katika hali ya kawaida.

“Tunafarijika kuona Rais Samia Suluhu Hassan, anafanya jitihada kuinua utalii, uhamasishaji wake utafanya wageni kuongezeka na bidhaa zetu zinaanza kuuzika kwa kiasi kwani wateja wetu

ni wageni kutoka nje” anaeleza Nkwikwi.

Aidha ametaka watu kupenda kununua bidhaa za uchoraji na vinyago ili kuendeleza utamaduni wetu wa Kitanzania.

“Watanzania hawana utamaduni wakununua bidhaa hizi, ila zinamaana kubwa katika makabila yetu, licha ya kuwa ni mapambo, vinyago na picha hubeba maana mbalimbali zinazowakilisha jamii zetu.

Inashangaza kuona tunategemea wazungu kuja kununua mambo yanayohusiana na utamaduni wetu kuliko sisi wenyewe,” anasema.

Aidha Nkwikwi, amewaomba wasanii wa fani hizo kujituma katika kazi na kuamini matunda ya yataonekana licha ya kupitia katika kipindi kigumu.



# Unayajua mataifa yanayotunishiana misuli duniani miaka nenda rudi?

## ●Kila kukicha hofu silaha za maangamizi
## ●Maisha yao 'huyu akija na hili,yule lile'

**Na Mwandishi Wetu**

IMEKUWA kawaida kuona taifa moja na lingine yakiwa katika uhusiano mzuri wa kidiplomasia.

Mataifa yakiwa katika mfumo huo wa mawasiliano ni jambo linalotajwa kusaidia sana kuepusha mifarakano na kurahisisha shughuli na utendaji wa kimataifa, baina ya nchi husika.

Licha ya kuwapo juhudi za kimataifa, yapo mataifa machache ambayo hayajawahi kuwa na uhusiano mzuri baina yao na mara kadhaa kunatokea mtikisiko wa uhusiano wao kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Je unayajua mataifa hayo hasimu duniani? Shirika la Habari la Uingereza (BBC) limetoa orodha ya mataifa hasimu, ambayo kwa muda mrefu uhusiano wao kidiplomasia ni sawa na ule wa paka na panya.

**MAREKANI NA URUSI**

Marekani ni nchi inayoongoza kuzozana na mataifa mbalimbali kama maslahi yake yakiguswa. Ukiacha China, ambayo ipo katika mzozo wa kiuchumi, Urusi ndiyo nchi hasimu pekee inayoonyesha misuli. Walianza kuhasimiana tangu kujiingiza kwao kwenye migogoro ya nchi za Vietnam na Afghanistan. Hata baada ya vita baridi kumalizika miaka ya hivi karibuni, kwa sasa kila nchi inajihami kwa silaha kali, dhidi ya mwenzie.

**ISRAEL NA PALESTINA**

Uhasama huu unaonekana kirahisi zaidi kwa kuwa uko wazi licha ya kuichanganya dunia. Mzozo wa kihistoria kati ya Waarabu na Wayahudi umedumu kwa muda mrefu sana hasa katika eneo la Jerusalem. Juhudi zinafanyika kupatanisha hazijafua dafu, lakini historia inarejesha machungu yanayoleta ugumu wa kupatikana kwa suluhu ya kudumu.

**CHINA NA JAPAN**

Nchi hizi zilianza uhasama na kupigana tangu mwaka 663. Hata baada ya vita kuu ya pili ya dunia, Japan iliivamia China na kutwaa maeneo mengi ya nchi hiyo. Katika uvamizi huu, inaelezwa ukatili mwingi ulifanyika ikiwamo matumizi ya silaha za kemikali, mauaji ya halaiki na ubakaji.

Mpaka leo kuna mzozo wa mipaka baina ya nchi hizo, huku China ikiendelea kuituhumu Japan kwa kushindwa kukiri makosa yake ya huko nyuma.

**IRAN NA SAUDI ARABIA**

Mashariki ya kati kunazidi kuwaka moto kutokana na mzozo wa kisiasa uliopo kati ya mataifa haya makubwa katika ukanda huo. Hata hivyo, Iran na Iraq chini chini kuna fukuto, lakini bado Saudi Arabia imekuwa adui mkubwa wa taifa hilo.

Nchi hizi zote ni za kiislamu, Saudi Arabia ni chimbuko la Wasunni na Iran ni chimbuko la Washia, lakini hawawezi kukaa kiti kimoja kutokana na kila mmoja kuwa na msimamo mkali, dhidi ya mwenzake.

Kinachowazozanisha mataifa haya ni masuala matatu makubwa, ambayo ni mafuta, gesi na nani anauhusiano gani au anaungwa mkono na mataifa ya Magharibi.

Saudi Arabia ina urafiki na nchi kama Uingereza na Marekani, ambao ni mahasimu wa Iran.

**KOREA KASKAZINI NA KOREA KUSINI**

Hizi zilikuwa nchi moja, lakini baada ya vita ya pili ya dunia, zilitengana rasmi, huku Wasoviet wakiiunga mkono Korea Kaskazini na Marekani ikiisaidia Korea Kusini.

Mwaka 1950, Korea Kaskazini ilitangaza viti, dhidi ya Korea Kusini, vita ambayo iliwahusisha pia Marekani na China. Uhusiano wao kwa sasa umeimarika hasa katika miaka ya hivi karibuni, ila wengi wanatazama kama uhusiano wa kuwindana.

**INDIA NA PAKISTAN**

Uhasama wa mataifa haya unajengwa zaidi na mambo mawili, tofauti ya mitizamo ya imani kati ya Wahindu na Waislamu pamoja na mgogoro wa mipaka.

Mara kadhaa kumezuka mapigano baina ya nchi hizo ikiwamo vita kubwa ya mwaka 1965, na 1971. Kwa sasa nchi zote mbili zinamiliki kiwango kikubwa cha silaha za nyuklia, kwa lengo la kujilinda dhidi ya mwenzake.

Wataalamu wa masuala ya usalama wana wasiwasi kwamba huenda kukazuka vita kubwa itakayohusisha silaha ya nyuklia baina ya nchi hizi.

**UINGEREZA NA UFARANSA**

Pamoja na kuwa vinara katika Umoja wa Ulaya, lakini bado zinahasimiana na kutazamana vibaya muda wote.

Uhasama wa nchi hizi ni wa kihistoria, ulianza tangu karne ya 10, ambapo wafalme wa nchi zote, walizozania ardhi ya upande wa pili. Katika Karne hiyo William wa Normand, aliyekuwa chini ya Mfalme wa Ufaransa alivamia Uingereza, baadae waingereza walipaswa kuachia mali zote kutoka Urithi wa Wanormandi. Igawa kwa sasa uhusiano wao nje ya sura ya kimataifa si wa mashaka sana, lakini historia inawaweka kwenye mataifa hasimu yasiyokubaliana.

**UTURUKI NA UGIRIKI**

Uhasama wao ulianzia mwaka 1954, wakati himaya ya Byzantine ilipovamiwa na himaya ya kiflame ya Kituruki ya Ottoman. Baada ya Ugiriki kupata uhuru, 1832. watu wa Ottoman, waliendelea kupambana kurejesha himaya hiyo kiasi cha kuwaingiza kwenye vita ya dunia ya kwanza.

Hata baada ya vita ya kwanza ya dunia kumalizika, pande hizo ziliendelea kutwangana. Mpaka leo mihemko baina ya nchi hizo zinasalia kwenye mioyo ya wananchi zinaendelea kutikisa.

**UINGEREZA NA IRELAND**

Hawa ni ndugu wanaogombana chumbani, wakitoka nje wanatabasamu.

Uhusiano wao ulianza kutetereka tangu miaka mingi, licha ya kuwa na mahusiano kisiasa tangu karne ya 16 na kuwa nchi moja kuanzia mwaka 1801, kumekuwa na uhasimu unaotokana na Ireland kutaka kuwa nchi huru. Ukiacha eneo la Ireland ya Kaskazini, eneo kitovu cha Ireland lilijitenga na Uingereza mwaka 1921. Uhasama haukuishia hapo umejitokeza hata hivi karibuni tu wakati Uingereza ikitangaza kujitoa katika Umoja wa Ulaya.

**UJERUMANI NA UFARANSA**

Nchi hizi ni majirani, kila mmoja akitupa lawama kwa kilichotokea miaka ya huko nyuma. Ufaransa inailaumu Ujerumani kwa kuwa sehemu ya chanzo cha vita kuu ya kwanza ya dunia.

Katika vita kuu ya pili ya dunia, wafaransa wengi aliingia kwenye mtego wa Ujerumani na kushikiliwa na vikosi vya jeshi chini ya Hitler.

Hata hivyo uhusiano wao sasa umeimarika kiasi cha kusahau machungu yaliyojitokeza kihistoria.

**Kwa msaada wa mtandao.**





# Mzazi adai dola milioni 1 binti yake kunyolewa nywele shuleni

**Michigan,** MAREKANI

BABA mmoja anadai alipwe dola milioni moja, baada ya binti yake mwenye umri wa miaka Saba, kukatwa nywele na mwalimu wake, shuleni.

Jimmy Hoffmeye, raia wa Marekani anaishitaki shule ya mtoto wake pamoja na wafanyakazi wake wawili kwa kukata nywele za binti yake bila ruhusa ya mzazi.

Kulingana na mashitaka yake, Jimmy Hoffmeyer anasema haki ya mtoto wake ya kuwa na nywele ilikiukwa na ameamua kumhamisha mtoto wake katika shule hiyo.

Uchunguzi uliofanywa kuhusiana na kisa hicho, ulibaini kuwa licha ya kumnyoa nywele, mwalimu huyo pia alimbagua kwa misingi ya rangi yake.

Mwalimu huyo alipatikana na hatia ingawa aliendelea kufanya kazi katika shule ya Ganiard iliyopo Michigan.

Mashitaka dhidi ya shule na wafanyakazi wake wawili kumuhusu msichana Jurnee yalipelekewa katika Mahakama ya Michigan. **BBC**

# Naibu Waziri Mkuu Taliban akanusha uvumi kifo chake

**Kabul,** AFGHANISTAN

NAIBU Waziri Mkuu wa Afghanistan, Mullah Baradar Akhnund, siku ya Jumatano alijitokeza kwenye televisheni ya taifa, kukanusha uvumi kwamba alijeruhiwa au kuuawa katika mapambano ya ndani ya kundi la Taliban.

Katika mahojiano mafupi, Baradar alisema alikuwa safarini katika eneo la nje ya Kabul na hakuwa na mawasiliano yoyote kuweza kuzungumza na watu ili kuwahakikishia juu ya hali yake.

Alisema Wataliban hawakuwa na mapambano yoyote miongoni mwao kwa ajili ya madaraka au nafasi, wanapambana tu kukomesha ukaliaji wa Afghanistan.

Hivi karibuni, zilizuka ripoti kwamba uongozi wa Taliban haukuridhishwa kwa pamoja na muundo wa baraza la mawaziri, kwa sababu mamlaka makubwa zaidi yalitolewa kwa mtandao wa Haqqan na kusababisha mapambano ya vurugu ya ndani.

Kulikuwepo hata na uvumi kwamba Baradar alikuwa ameuawa au kujeruhiwa.

**DW**

# Ruto akubali kupatanishwa na Uhuru

**Nairobi,** KENYA

NAIBU Rais wa Kenya, William Ruto, ameafiki nia ya Maaskofu wa Kanisa Katoliki Kenya ya kumpatanisha na Rais Uhuru Kenyatta, limeripoti gazeti la Daily Nation nchini humo.

Katika mazungumzo na viongozi wa kidini wa mashinani nyumbani kwake eneo la Karen Nairobi, Ruto alisema yuko tayari na ana utashi wa kukutana na Rais Kenyatta.

Ruto alisema uhasama baina yake na rais ulisababishwa na watu kutoka nje ambao walitaka kunufaika na serikali ambayo hawakuiunda.

"Huwezi kudoea serikali ambayo hukuunda," aliongeza Ruto akisema kuwa makubaliano ya Machi 2018 yanayofahamika kama 'handshake' baina ya kiongozi wa chama cha upinzani cha ODM Raila Odinga na Rais Kenyatta yalikuwa chanzo.

"Kuna watu wakasema huyu deputy president kwanza tuweke kando. Lakini mimi niko tayari wakati wowote bila masharti," limenukuu gazeti la citizen nchini humo.

Mzozo baridi umekuwa ukiendelea baina ya kambi ya rais Uhuru Kenyatta na ile ya Naibu rais William Ruto baada ya makubaliano baina ya Rais Kenyatta na kiongozi mkongwe wa upinzani yaliyoitwa 'Handshake'.

Upande wa Rais Kenyatta unadai kuwa 'handshake' ilihusu makubaliano ya kurejesha umoja miongoni mwa Wakenya na hivyo kukomesha ghasia za kikabila zinazoibuka hususan kila baada ya uchaguzi.

Hata hivyo Ruto anadai kuwa hakuhusishwa katika makubaliano hayo, na amekuwa akitengwa na Kenyatta katika masuala mbali mbali ya kitaifa baada ya 'Handshake'.

**BBC**




Wanajeshi wa Urusi wakipanga foleni kwa ajili ya kupiga kura ya uchaguzi wa bunge Rostov-on-Don, jana. Kwa siku tatu Urusi inafanya uchaguzi huo. **PICHA: AP**

# ECOWAS yawawekea vikwazo wanajeshi waliofanya mapinduzi

**Accra,** GHANA

JUMUIYA ya Kiuchumi ya nchi za Magharibi mwa Afrika (ECOWAS), imewawekea vikwazo vya safari na fedha, kikosi cha wanajeshi waliopindua serikali ya Guinea, pamoja na familia zao.

Uamuzi huo, umetangazwa baada ya kikao maalumu cha jumuiya hiyo, kilichofanywa katika mji mkuu wa Ghana, Accra.

Vikwazo hivyo vinatarajiwa kuongeza shinikizo kwa wanajeshi hao kurejesha utawala wa Katiba.

Pia umoja huo unalitaka jeshi kufanya uchaguzi ndani ya miezi sita na kusisitiza kuwa hakuna kiongozi yeyote atakayeruhusiwa kugombea katika uchaguzi huo.

Viongozi hao hata hivyo wameeleza utayari wao wa kuiunga mkono Guinea katika mchakato huo wa mpito.

Wametoa wito kwa Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Mataifa (UN) na washirika wao wa kimataifa kusaidia utekelezaji wa marufuku ya kusafiri na vikwazo vya fedha dhidi ya wanajeshi hao na familia zao.

Wanataka pia kutolewa bila masharti kwa Rais aliyeondolewa mamlakani Alpha Condé.

**BBC**

# China jeshi la pamoja dhidi yake

**Hongkong,** CHINA

CHINA imelaani ushirika mpya wa usalama wa kihistoria kati ya Marekani, Uingereza na Australia.

China imeutaja muungano huo kuwa wenye maono yasiyofaa.

Makubaliano hayo yatazifanya Marekani na Uingereza kuipatia Australia teknolojia ya kujenga manowari zenye uwezo wa kinyuklia kwa mara ya kwanza.

Kuundwa kwa muungano huu inaonekana kama juhudi za kuukabili ushawishi wa China katika eneo la Kusini mwa China linalozozaniwa.

Wakati huo huo Umoja wa Ulaya (EU), umesema haukufurahishwa kuhusu kuundwa kwa ushirika mpya wa kijeshi kati ya Marekani, Uingereza na Australia, kwa mujibu wa msemaji wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya Peter Stano, huku akiongeza kwamba watajaribu kuzungumza na Marekani, Uingereza na Australia ili kujua kinachoendelea.

Peter Stano amebaini kwamba nchi za Ulaya zitajadiliana kuhusu athari ya uamuzi wa nchi hizo tatu.

Viongozi wa Marekani, Uingereza na Australia wameutangaza ushirika huo mpya, ili kuzuia kile kinachotafsiriwa kama hatua ya kukabiliana na ushawishi wa China unaozidi kupanuka katika ukanda wa Indo-Pasifiki.

**RFI**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**


Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAIKIN TANZANIA LTD** INATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 283 CVE** TOYOTA **RAV 4.** YENYE CHASSIS NAMBA **ACA200031584.** ENGINE NAMBA 1AZ4140734. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MBU/RB/451668/2021.**

116467002

**IN THE DISTRICT LAND HOUSING TRIBUNAL FOR MARA AT MUSOMA**

**APPLICATION NO 76 0F 2021**

**SOPHERETI RUHUMBIKA.......................APPLICANT**

**VERSUS**

**SAID MUYA.........................................RESPONDENT**

**SUMMONS/NOTICE**

**TO, SAID MUYA**
The above mentioned applicant has instituted a suit at this court, against you, particulars of which are mentioned in a copy of application which is obtainable from the registry of this court, YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS COURT in persons (s) or by recognized agents (S) for mention/ hearing on 20th September, 2021, at 08: am in the fore noon.
**TAKE NOTICE THAT;**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned and determined in your absence.
**Given under my hand and seal of this Tribunal this 20 day of August, 2021.**

Kitungulu, E
Chairman
District Land and Housing Tribunal – Mara

116467202

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.......2021**

**In the Matter of the Estate of the late ERASTO MNYANYI KASUGA of NG'HONG'HONHA within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARTINA ERASTO MNYANYI**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30 Day of SEPTEMBER 2021.
Dated at Dodoma this 9TH day of September 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

116467102

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO.219/2017**

**ESTON DAUD SINDWANI::::::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**LUKAS S.AMILIKE:::::::::::::::::::::::::::: MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA : GURD STIVIN,**

**Fahamu kwamba ESTON DAUD SINDWANI amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.**

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 22/09/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tatehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka : Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

**Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 09/09/2021.**

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**09/09/2021**

116467502

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA**

**MAHAKAMA YA MWANZO MSOGA WILAYA BAGAMOYO,**

**SHAURI LA MADAI YA NDOA NA TALAKA NO. 03/2021**

**MDAI..................JUSTINE % MUSSA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA.........................JACKLIN % FRANK MWANYASI**

**KUITWA SHAURINI**
**JACKLIN % FRANK MWANYASI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya talaka, hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 30/09/2021 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 17/09/2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MSOGA - LUGOBA

116467602

## KUPOTEA KWA CHETI

**JENGA FAMILIA (JEFA)**
Inatangaza kupotea kwa cheti chake cha usajili chenye namba **s.a.17784.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. control number: **9910830269979.**

116466902

## KUPOTEA KADI YA BAJAJ

**PHILIPO D. MWAKALOBO**
ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **BAJAJ aina ya TVS** yenye namba za usajili **MC 803 BZQ**
Injini namba **AK4EJ4424762**
chasiss namba **MD6M14PA5J4E19780**
Mali ya kampuni ya **FAVOUR GENERAL SUPPLIES**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/453246/2021**

116467302


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Kesho mimi siondoki kabisa kule tunapoishi. Wewe nenda naye huko. Hakikisha anakunywa pombe na nyingine mnaondoka nayo, ili iwe rahisi kumwekea vidonge. Usikosee kitu chochote. Halafu usiruhusu akushikeshike sana..."

Wakati anaongea maneno hayo, Tedi alianza kuangua kicheko.

"Wivu huo sasa." Tedi alimtia singi.

Maneno hayo yalimfurahisha sana Tedi. Alishaanza kujua kuwa ameingia kwenye moyo wa Tom na kuanza kumuonea wivu.

"Tom niachie hii ngoma niicheze. Haambui kitu na mimi nitamuonyesha. Kwanza nina hasira naye. Hawezi kuwa anadhalilisha wanawake. Kila mwanamke anamtake yeye?"

Tom aliangua kicheko "Kusema kweli najivunia kuwa nawe Tedi. Kila siku zinavyozidi kwenda mbele, nagundua kuwa haukuwa mwanamke wa kusukuma siku zangu ziende hapa Morogoro, ila ni mtu muhimu na msaa mkubwa kwangu. Sikutarajia kuja huku na kupata msaada mkubwa kama huu, achilia mbali huu wa kuwa mpenzi wangu."

"Nashukuru baba. Sasa naona muda unazidi kwenda, tuondoke twende kwetu. Nimechoka na njaa inauma, sitaki kula hapa, nataka tukale kwetu. Kazi ya kwanza tumeimaliza vizuri. Basi hatua inayofuata."

"Nakuaminia Tedi. Sijui ukiikamilisha nitakubeba na mbeleko gani?"

"Yoyote ile." Alijibu na kucheka, huku wakiwa amesimama, tayari kwa kuondoka.

"Hata kaniki?" Aliuliza kimzaha Tom na kusababisha vicheko kwa wapenzi hao wawili waliokuwa wakitazamwa na wengi kwenye baa hiyo kwa jinsi walivyopendezana na kupendeza.

******************************

Tedi aliingia kwenye baa ya Deluxe. Kama alivyotegemea alimkuta Sam amejaa tena kama pishi la mchele.

"Umependeza kweli." Sam alichombeza.

"Wewe acha masihara yako." Alijibu.

"Kweli tena." Sam aliendelea. Halafu kama akakumbuka kitu hivi.

"Yule bwege umemuacha wapi?"

"Yupo nyumbani kwake." Tedi alijibu akiwa tayari ameshakaa.




**"Nashukuru baba. Sasa naona muda unazidi kwenda, tuondoke twende kwetu. Nimechoka na njaa inauma, sitaki kula hapa, nataka tukale kwetu. Kazi ya kwanza tumeimaliza vizuri. Basi hatua inayofuata."**

"Si nimesikia unaishi naye?" Sam alizidi kudadisi.

"Nani kakwambia na wewe. Yeye anaishi kwake na mimi kwangu."

Sam hakutaka kuendelea sana kwa sababu siyo lililomleta.

Alijua maswali mengi, yanaweza kukasirisha windo lake. Kwa kawaida Sam ni mpenda wanawake.

Mbali na kunywa pombe, lakini alihusudu mno vimwana. Kwenye baa ya Mwenda alimaliza karibuni mabaamedi wote. Wachache wao ambao bado alikuwa ni Tedi. Na wale ambao hajawapata ni wale ambao yeye hawahitaji.

Tedi ni mmoja wa wasichana mrembo ambao waliwatongoza kwa muda mreru, lakini aligonga mwamba.

Ni kwamba Tedi alionekana ni mwanamke aliyekuwa akichagua wanaume. Si kila mwanaume. Hii ilimjengea heshima kwenye baa ile. Wanaume wengi walimtaka. Walimtongoza. Wakagonga mwamba.

Wakabaki kumtazama. Kumtamani. Wengine walimtukana na kumdhihaki. Ni kwa sababu tu amewakataa.

Haikuwa hivyo kwa upande wa Tom. Tedi alimkubali ingawa ilikuwa ni mara ya kwanza kwa sababu kadhaa.

Kwanza aliyemtaka alikuwa ni mgeni, hivyo alijua atakwenda naye na kuondoka, hivyo heshime yake itaendelea kuwepo kwenye baa ile. Pili muhitaji alionekana ni mtu mkarimu na mstaarabu, tofauti na wengine waliokuwepo kwenye baa ile.

Hakuonekana kuwafokea, kuwanyanyasa, au kuwashikashika wahudumu kwa namna ya kuwadhalilisha.

Yeye ndiye alimhudumia. Alimwita kwa heshima. Akamsalimu. akaaongea maneno ya utani kidogo. Akamuagiza kinywaji.

Alipoleta baada ya kuzifungua, Tom alimshukuru Tedi. Na hata baadaye alipomwita, wakati akidhani anataka kumtuma tena. Alimpa noti ya shilingi elfu kumi, ambayo alikuwa hajawahi kupewa na mwanaume yoyote kwenye baa ile hivi hivi tu, ili akanunue anachokitaka.

Na ndiyo maana alipoletwa na mwenzake ili waupitishe usiku pamoja, hakukataa.

Kwa sasa hawaupitishi usiku tena. Wapo pamaoja kwa muda wa wiki nzima sasa.

"Tuondoke sasa." Alimuru Sam.

"Sawa beba na bia zingine tukanywe nyumbani kwako."

"Sawa, si nilikwambia yule bibie amekwenda Dar eee."

"Ndiyo jana ulinieleza."

*************************************

Haikuwa kazi kubwa sana kama alivyofikiri. Sam alikuwa ameshaelewa. Alichofanya Tedi ni ulaghai wa kimapenzi. Alimkumbatia kwa mahaba. Akamimina bia kwenye glasi, akamnyesha. Sam alijua amepata. Kumpata Tedi, msichana mrembo aliyeshindikana. Na kwa sasa amekuwa mrembo zaidi, kwani ni bahati kubwa.

Alijua kuwa kesho atakwenda kuwatambia wenzake. Kumpata mrembo aliyeshindikana, yeye ndiye atakuwa mshindi.

"Nenda basi kaoge, na mimi niende tuje kulala." alisema.

Lilikuwa ni kosa kubwa kwa Sam. Ni kosa la kiufundi.

Alipoingia bafuni. Haraka, Tedi alikwenda alifungua mkoba wake na kutoa kidonge alichopewa na Tom. Akakitumbukiza kwenye glasi ya bia ilikuwa nusu.

Alichofanya akaongeza bila nyingine na kujaza.

Aliporejea, Sam alivua nguo na kubaki na bukta. Bila kuuliza akanyanyua glasi ile ile na kuimimina kinywani.

Nusu dakika baadaye alianza kuona dabo dabo. Nusu nyingine aliyobaki akalala fofofo. Akaanza na kukoroma akitoa povu ambalo lilianza kumtisha hata muwekaji mwenyewe.

Hata hivyo alikumbuka maneno aliyoambiwa na Tom kuwa hatokufa, ila atalala usingizi kwa masaa kadhaa, halafu ataamka.

Kazi iliyofuata ambayo kwake ndiyo aliiona ni kubwa zaidi ni kutafuta vitu ambavyo vilihitajika.

Kwa bahati nzuri alijua nini kilihitaji kutafutwa na nini kuachwa. Tatizo ni muda wa kutafuta na mada gani vielelezo vitapatikana.

Ilimchukua nusu saa kusaka huku na huko. Lakini ni vielelezo vitatu tu ambavyo aliona huenda vinaweza kumsaidia Tom. Baada kuangaza huku na huko, akafanikiwa tena kupata vitu viwili ambavyo vinavyofanana na anavyohitaji aliyemwagiza. Mwisho kabisa akaifuata simu ya mkononi. Akachukua na kuweka kwenye mkoba wake.

Kazi ikawa imekwisha. Alitumia saa moja na dakika 40, tangu alipoingia kwenye nyumba ya Sam na kukamilisha kazi ile. Aliondoka kwa tahadhari ili asishtukiwe na mtu yoyote. Ilikuwa ni saa sita na dakika ishirini usiku.

Alipotoka alitembea hatua kadhaa. Akasimamisha bodaboda na kuelekea anakoishi na mpenzi wake Tom.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

MECHI KALI
HOME
BURNLEY
3.66 | 3.32 | 2.08
ARSENAL
AWAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RASHFORD AREJEA MAZOEZINI UNITED



**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Marcus Rashford, ameonekana mazoezini wakati timu hiyo ikijiandaa na mwendelezo wa mechi za Ligi Kuu England wikiendi hii.

Rashford alifanyiwa upasuaji wa bega Julai, mwaka huu na taarifa rasmi kutoka United ziliripoti mchezaji huyo atarejea uwanjani mwishoni mwa Oktoba au mwanzoni mwa Novemba, 2021.

Kurejea kwa Rashford wakati huu, ni mapema kuliko ilivyokuwa imetarajiwa na hii ni ishara nzuri kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer na kikosi cha United kwa ujumla.

Ingawa bado ni mapema kumwona Rashford uwanjani, mashabiki wa Mashetani Wekundu hao wategemee kumwona mshambuliaji huyo muda mfupi ujao akichuana na washambuliaji wenzake kwenye kikosi cha timu hiyo.

United watasafiri wikiendi hii kuwafuata West Ham United pale kwenye Uwanja wa London katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Timu hizi zitakutana tena Jumatano wiki ijayo kwenye mzunguko wa tatu wa Kombe la Carabao, kabla ya United kuwaalika Villareal kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# GREALISH SASA TAMBO KIBAO



**MANCHESTER, England**

JACK Grealish nyota mpya ndani ya kikosi cha Manchester City ambaye alisajiliwa akitokea Klabu ya Aston Villa ameweka wazi anauwezo wa 'kumpindua' beki wa aina yoyote akiwa anakimbia ndani ya boksi.

Hii inatokana na bao lake alilofunga kwa kuwachambua mabeki kadhaa na kuiwezesha Manchester City kushinda mabao 6-3 dhidi ya RB Leipzig kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatano.

Kiungo huyo mwenye miaka 26 alikuwa akicheza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwwa Ulaya ndani ya Uwanja wa Etihad.

Na sasa ameelezea namna alivyokuwa na furaha kwa kufunga kwenye mchezo huo.

"Mpira ulikuja kwangu na ninapokuwa katika nafasi hiyo nikikimbia ninaweza nikampita yeyote tukikabiliana mmoja mmoja, nina furaha kupata bao," alisema akinukuliwa na Sky Sport.

"Kwa hakika ilikuwa furaha kubwa zaidi ndani ya moyo wangu na nina amini nitaendelea kufunga kwenye kila mechi zinazokuja."

## HABARI MICHEZO

# ,059,740 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 18.9.21 | 17:00 | Derby vs Stoke City | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 2. 18.9.21 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 3. 18.9.21 | 17:00 | Cardiff vs Bournemouth | 2.86 | 3.31 | 2.36 |
| 4. 18.9.21 | 17:00 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 5. 18.9.21 | 18:00 | Lens vs Lille | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 6. 18.9.21 | 19:30 | Aston Villa vs Everton | 2.46 | 3.27 | 2.92 |
| 7. 18.9.21 | 19:30 | Elche vs Levante | 2.67 | 3.13 | 2.77 |
| 8. 18.9.21 | 22:00 | Alaves vs Osasuna | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 9. 19.9.21 | 13:30 | Empoli vs Sampdoria | 2.52 | 3.63 | 2.62 |
| 10.19.9.21 | 14:00 | Nice vs Monaco | 2.73 | 3.38 | 2.48 |
| 11. 19.9.21 | 16:00 | Brighton vs Leicester | 2.83 | 3.19 | 2.58 |
| 12. 19.9.21 | 17:15 | Real Sociedad vs Sevilla | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 13. 19.9.21 | 21:45 | Juventus vs AC Milan | 2.36 | 3.32 | 3.03 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 18 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3354 | Hull City vs Sheffield Utd | 3.10 | 3.25 | 2.25 |
| 14:30 | 3742 | Wolverhampton vs Brentford | 1.87 | 3.27 | 4.63 |
| 15:00 | 1276 | Rayo Vallecano vs Getafe | 2.45 | 2.92 | 3.28 |
| 16:00 | 1722 | Kasimpasa vs Trabzonspor | 3.65 | 3.70 | 1.88 |
| 16:00 | 1988 | Toulouse vs Grenoble Foot | 1.68 | 3.51 | 5.14 |
| 16:00 | 2913 | Sochaux vs Paris FC | 2.42 | 3.10 | 2.95 |
| 16:00 | 3505 | Genoa vs Fiorentina | 3.31 | 3.31 | 2.22 |
| 16:30 | 3385 | Kryliya Sovetov vs Rostov | 2.12 | 3.26 | 3.36 |
| 16:30 | 3689 | Mainz vs SC Freiburg | 2.02 | 3.53 | 3.48 |
| 16:30 | 3790 | Arminia Bielefeld vs Hoffenheim | 3.44 | 3.49 | 2.05 |
| 16:30 | 4096 | Augsburg vs Monchengladbach | 3.93 | 3.88 | 1.81 |
| 16:30 | 5746 | Bayern Munchen vs VfL Bochum | 1.06 | 11.90 | 25.79 |
| 17:00 | 1025 | Huddersfield vs Nottingham | 2.05 | 3.29 | 3.54 |
| 17:00 | 1142 | QPR vs Bristol City | 1.79 | 3.70 | 4.04 |
| 17:00 | 1733 | Hibernian vs St Mirren | 1.61 | 3.75 | 5.33 |
| 17:00 | 1994 | Ross County vs Hearts | 4.42 | 3.78 | 1.71 |
| 17:00 | 2613 | Liverpool vs Crystal Palace | 1.22 | 6.43 | 12.05 |
| 17:00 | 2833 | Norwich City vs Watford | 2.16 | 3.31 | 3.46 |
| 17:00 | 2835 | Aberdeen vs St Johnstone | 2.04 | 3.05 | 3.88 |
| 17:00 | 3110 | Burnley vs Arsenal | 3.66 | 3.32 | 2.08 |
| 17:00 | 3262 | Manchester City vs Southampton | 1.19 | 6.82 | 13.99 |
| 17:00 | 4323 | Middlesbrough vs Blackpool | 1.77 | 3.45 | 4.53 |
| 17:00 | 4612 | Fulham vs Reading | 1.36 | 4.83 | 7.50 |
| 17:00 | 4644 | Luton Town vs Swansea | 2.07 | 3.26 | 3.50 |
| 17:00 | 5036 | Derby vs Stoke City | 2.96 | 3.06 | 2.44 |
| 17:00 | 5067 | Cardiff vs Bournemouth | 2.81 | 3.25 | 2.43 |
| 17:00 | 5130 | Preston vs West Bromwich | 3.70 | 3.45 | 1.94 |
| 17:00 | 5213 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.07 | 2.57 |
| 17:00 | 5333 | Peterborough vs Birmingham | 3.20 | 3.30 | 2.18 |
| 17:00 | 5617 | SC Dnipro 1 vs Veres Rivne | 1.44 | 4.16 | 6.19 |
| 17:00 | 5863 | Millwall vs Coventry | 2.46 | 3.10 | 2.90 |
| 17:15 | 5636 | Atletico Madrid vs Athletic Bilbao | 1.68 | 3.56 | 5.62 |
| 17:30 | 4083 | Famalicao vs Maritimo | 2.02 | 3.30 | 3.60 |
| 17:30 | 4091 | Heerenveen vs Fortuna Sittard | 1.72 | 3.88 | 4.23 |
| 18:00 | 3845 | Lens vs Lille | 2.54 | 3.28 | 2.73 |
| 19:00 | 1303 | Inter vs Bologna | 1.38 | 5.20 | 7.21 |
| 19:00 | 3534 | Antalyaspor vs Besiktas | 4.44 | 3.65 | 1.74 |
| 19:00 | 4239 | Adana Demirspor vs Caykur Rizespor | 1.85 | 3.56 | 3.95 |
| 19:30 | 1000 | Aston Villa vs Everton | 2.37 | 3.32 | 3.02 |
| 19:30 | 1377 | FC Koln vs RB Leipzig | 4.18 | 3.98 | 1.74 |
| 19:30 | 1519 | Elche vs Levante | 2.42 | 3.11 | 3.11 |
| 19:45 | 3965 | Willem II Tilburg vs Groningen | 2.39 | 3.31 | 2.82 |
| 20:00 | 1841 | Belenenses vs Gil Vicente | 3.45 | 3.06 | 2.18 |
| 20:30 | 3182 | PAS Giannina vs Panathinaikos | 3.20 | 3.35 | 2.16 |
| 21:00 | 1349 | Ajax vs Cambuur | 1.08 | 9.91 | 20.81 |
| 21:45 | 3393 | Salernitana vs Atalanta | 9.03 | 5.62 | 1.30 |
| 22:00 | 2570 | Utrecht vs Waalwick | 1.29 | 5.53 | 8.29 |
| 22:00 | 3206 | St Etienne vs Bordeaux | 1.93 | 3.44 | 3.89 |
| 22:00 | 5695 | Alaves vs Osasuna | 3.01 | 3.01 | 2.56 |
| 22:30 | 2965 | FC Arouca vs Vitoria Guimaraes | 3.64 | 3.39 | 1.98 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MADRID, PSG ZAMGOMBEA RUDIGER




**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeanza mazungumzo na nyota wake Antonio Rudiger na suala kubwa ni kuhusu kuongeza mkataba wake, lakini Sky Sport imeripoti nyota huyo anawaniwa na PSG pamoja na Real Madrid.

Chelsea imeweka wazi kuwa inahitaji kuona nyota huyo anabaki ndani ya kikosi chake.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, PSG na Real Madrid zinamtazama kwa ukaribu nyota huyo ili ziweze kupata huduma yake.

Mabosi hao wa Ulaya wapo tayari kumpa dili nyota huyo ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika ifikapo mwakani.

Kocha Thomas Tuchel ameweka wazi hana mpango wa kuendelea kuwa naye kwenye kikosi hicho.

Rudiger mwenyewe bado hajaonyesha nia ya kutaka kuendelea kubaki kwenye kikosi hicho, huku mazungumzo baina ya pande hizo mbili yakiendelea.




# FOFANA: NATAMANI KUICHEZEA MADRID

**LONDON, England**

MLINZI wa kati wa Leicester City, Wesley Fofana amesema ni ndoto yake kuichezea Real Madrid siku moja.

Fofana amejitambulisha kama mmoja wa mabeki wachanga katika soka la Ulaya tangu alipojiunga Ligi Kuu England na ametangaza nia yake kwa siku moja kufuata nyayo za rafiki yake Eduardo Camavinga kwa kuhamia kwenye mji mkuu huo wa Hispania.

"Uvumi wa Real Madrid?" alisema katika mahojiano kwenye YouTube.

"Ni heshima, Real Madrid ndio klabu ya ndoto zangu.

"Ni klabu kubwa zaidi ulimwenguni na ndoto yangu ni kucheza huko."

Fofana kwa sasa ameumia hadi kuanza kwa mwaka 2022, baada ya kuvunjika mguu katika mechi ya kirafiki ya kabla ya msimu na Villarreal.

Ameng'aa katika kikosi hicho cha Brendan Rodgers tangu aliposajiliwa na klabu hiyo katika msimu wa joto wa 2020 kwa mkataba wa euro milioni 35 kutoka Saint-Etienne.

Real Madrid tayari wamemtambua Mfaransa huyo kama mlengwa wa siku zijazo. Ukweli kwamba ametangaza wazi mapenzi yake kwa klabu itasaidia katika mazungumzo yajayo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO HATACHEZA MFULULIZO- SOLSKJAER

●●●Lakini ni ngumu kumweka benchi nyota huyo kutokana na kuwa na mwanzo mzuri...

**MANCHESTER, ENGLAND**

RONALDO alifurahia kurudi kwa mara ya pili Manchester United kwa kufunga katika mechi tatu mfululizo, akifunga mbili za Ligi Kuu England na moja ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hatacheza kila mechi kwa mujibu wa Ole Gunnar Solskjaer.

Kocha huyo amesisitiza "haiwezekani" kumweka Ronaldo nje, lakini ni vigumu kumchezesha kila mechi msimu huu kufuatia mwanzo mzuri ndani ya dimba la Old Trafford.

"Ronaldo ni ngumu kumwacha nje, lakini ukweli uliowazi kuwa hatacheza kila mechi," alisema Solskjaer akinukuliwa na Daily Mail.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliyeondoka mwaka 2009 hapo Manchester United na kuhamia Real Madrid kabla ya kwenda Juventus na kurudi tena Old Trafford.

United ilikumbana na kipigo cha kwanza msimu huu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati ilipokubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Young Boys ya Uswisi.

"Haiwezekani kumweka nje," Solskjaer alisema.

"Ronaldo ana miaka 36 wakati Mason (Greenwood) ana miaka 19, inabidi niweze kuangalia muda wake na umri wake."

Ronaldo amekuwa ni mchezaji mwenye umri mkubwa kufunga mara mbili katika Ligi Kuu England nyuma ya Graham Alexander wa Burnley dhidi ya Hull City mwaka 2010.

Alexander alikuwa na umri wa miaka 38 na siku 182 wakati akifanya hivyo.

## ZISIKUPITE

### BARCA WAMTAKA POGBA
BARCELONA ina matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba katika uhamisho wa bila malipo msimu ujao iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ataamua kukataa kuongeza kandarasi mpya pale Old Trafford. Pogba pia anawaniwa na PSG, Juventus na Real Madrid. **(Fichajes)**

### WERNER KUMRITHI HAALAND
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25 ni miongoni mwa wachezaji wanne wanaonyatiwa na Borussia Dortmund iwapo mshambuliaji matata wa klabu hiyo, Erling Braut Halaand ataondoka katika klabu hiyo msimu ujao. **(SportBild)**

### RUDIGER MAMBO MAGUMU
MKABATA wa beki wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger katika klabu ya Chelsea unakamilika msimu ujao na mazungumzo ya kuuongeza yamegonga mwamba. **(Times)**

### ARTETA KUMBEBA PATINO
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anatarajiwa kumkuza kiungo wa kati wa timu ya wachezaji chipukizi katika klabu hiyo, Charlie Patino katika kikosi cha kwanza, huku kukiwa na ripoti kwamba Barcelona inamnyatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17. **(Mirror)**

### VLAHOVIC KIZUNGUMKUTI
MMLIKI wa klabu ya Fiorentina, Rocco Commisso hajui iwapo mshambuliaji wa Serbia Dusan Vlahovic (21), ambaye amehusishwa na klabu za Manchester City, Atletico Madrid na Juventus, ataongeza mkataba wake zaidi ya Juni, 2023 na klabu hiyo ya Italia. **(Calciomercato, via Goal)**

### JONES, GAYLE KIMEUMANA
KOCHA Msaidizi wa Newcastle, Graeme Jones na mshambuliaji wa England, Dwight Gayle mwenye umri wa miaka 30, walirushiana maneno makali katika uwanja wa mazoezi huku nahodha, Jamaal Lascelles akilazimika kuingilia kati kwa kuwatawanya wawili hao. **(Mail)**

### BENITEZ ASAKA BEKI
KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amejipa kipaumbele kumsajili beki wa kati katika dirisha la uhamisho la Januari. **(Football Insider)**

### KOEMAN NJIA PANDA
BAADHI ya wajumbe wa Bodi ya Barcelona wamemtaka rais wa klabu hiyo, Joan Laporta kumfuta kazi Kocha, Ronald Koeman baada ya kufungwa mabao 3-0 na Bayern nyumbani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. **(AS)**

### SPURS YAMTAKA GINTER
KLABU ya Tottenham Hotspur ina hamu ya kumsajili mchezaji wa Borussia Monchengladbach, Matthias Ginter lakini inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Bayern Munich na Real Madrid ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na raia wa Ujerumani. **(Calciomercato)**

### ISAK AGOMBEWA EPL
BAADHI ya klabu za Ligi Kuu England, zinamnyatia mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, mwenye umri wa miaka 21, licha ya mchezaji huyo kukubali kusaini mkataba wa muda mrefu na Real Sociedad. Arsenal na Chelsea awali zimeonyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo. **(Fichajes via Teamtalk)**

### TIMBER ANUKIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imefungua mazungumzo na Ajax kuhusu uwezekano ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Uholanzi mwenye umri wa miaka 20, Jurrien Timber. **(Todofichajes)**

HABARI MICHEZO

# MANGALO NJE BIASHARA IKIWAKABILI WADJIBOUTI

**Na Shufaa Lyimo**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho, Biashara United wanatarajia kuwakaribisha Dikhil FC katika mchezo wa marudiano wa michuano hiyo utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza iliyofanyika wiki iliyopita nchini Djibouti, Biashara United inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ilipata ushindi wa bao 1-0.

Mechi hiyo inatarajiwa kuchezwa kuanzia saa 1:00 usiku (saa za Afrika Mashariki).

Bao la Biashara United katika mchezo wao wa kwanza lilifungwa na straika wake chipukizi, Denis Nkane.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Biashara United, Frank Wabale alisema kikosi chake kimeendelea kufanya mazoezi yake vyema lakini kitawakosa wachezaji wake nyota watatu ambao ni majeruhi.

Wabale aliwataja wachezaji hao watakaokosekana ni pamoja na Abdulmajid Mangaro, Baron Okech na Mghana Opare Collins.

Alisema kuelekea mechi hiyo wamejipanga vizuri kwa ajili ya kuhakikisha wanashinda mchezo huo na kusonga mbele katika michuano hiyo ambayo wanashiriki kwa mara ya kwanza.

"Tunaamini mchezo utakuwa na ushindani kutokana na ubora wa kila timu, hivyo tunawataka wachezaji wetu kuingia uwanjani kwa tahadhari kubwa," alisema Wabale.

Aliongeza licha ya kuwakosa wachezaji wao tegemeo, wamejipanga kupambana kuhakikisha wanaipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

Nkane aliliambia gazeti hili jana amejiandaa kucheza katika kiwango cha juu katika mechi hiyo ili kuisaidia timu yake kusonga mbele.

"Nimejiandaa na nimejipanga vizuri, nina matumaini ya kuendelea kucheza soka la ushindani," alisema Nkane.

Timu nyingine za Tanzania Bara zinazokabiliwa na mashindano ya kimataifa wikiendi hii ni pamoja na Yanga itakayokuwa ugenini Nigeria dhidi ya Rivers United wakati Azam FC yenyewe itavaana na Horseed utakaochezwa leo jijini.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (wa pili kulia), akipokea vifaa vya michezo kutoka kwa Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, kwa ajili ya kushiriki NMB Marathon 2021 zitakazofanyika Septemba 25, mwaka huu jijini Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa Uwajibikaji kwa Jamii, Lilian Kisamba na kushoto ni Meneja wa Biashara za Serikali, Irene Masaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB Marathon kusaidia Fistula

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, ameipongeza Benki ya NMB kwa kubuni jambo lililolenga kuimarisha afya za vijana na Watanzania kwa ujumla ambayo ni NMB Marathon 2021 'Mwendo wa Upendo'.

Akizungumza ofisini kwake jijini jana baada ya kupokea vifaa vya kukimbilia kutoka kwa wafanyakazi wa NMB, Gondwe alisema mbali ya kuimarisha afya, benki hiyo imeonyesha kuwathamini wanawake wenye ugonjwa wa Fistula ambapo sehemu ya fedha zitakazopatikana katika mbio hizo zitatumika kuwatibu.

"Nampongeza Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB pamoja na timu yake kwa kufikiria afya ya kinamama, unapomkumbuka mama maana yake umegusa nchi, unapoigusa nchi umegusa maendeleo. Hii marathon ina maana kubwa katika wilaya yangu, vijana wapenda michezo na wananchi wengine waje kwa wingi," alisema Gondwe.

Alisema NMB inawapenda watu wanaowazunguka, ndio maana wamefikiria badala ya kusubiri waugue waende kutibiwa hospitali kwa gharama kubwa wanakuja na suluhu ya kufanya mazoezi na kushiriki michezo ili kulinda afya zao.

"Naamini siku ya Septemba 25, mwaka huu watakuja wengi katika mbio hizi, mimi nawaambia nipo tayari kushiriki na nimeshapokea vifaa vya kazi, tukutane kwenye NMB Marathon 2021 "Mwendo wa Upendo," alisisitiza Gondwe.

Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema benki hiyo inatambua umuhimu wa afya bora lakini pia wanathamini mchango wa wanawake katika jamii.

"Kila siku tunatafuta namna ya kurejesha tabasamu kwa wateja wetu, tunahakilisha changamoto katika jamii zinapungua au kupotea kabisa. Hizi mbio mbali ya kuimarisha afya lakini pia zinaleta matumaini," alisema Richard.

## Ligi Kuu Zanzibar kuanza Oktoba 25

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), imetangaza rasmi kuwa msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2021/2022 utaanza ifikapo Oktoba 25, mwaka huu.

Akizungumza kwa niaba ya Makamu Mwenyekiti wa ZBL, Mohamed Massoud, mjumbe wa bodi hiyo alisema ligi hiyo itafunguliwa na mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Oktoba 23, mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema mechi hiyo ya Ngao ya Jamii itawakutanisha mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM dhidi ya Mafunzo.

Alisema dirisha la usajili litafunguliwa kuanzia keshokutwa Jumatatu na litafungwa ifikapo Oktoba 11, mwaka huu na usajili huo utafanyika kwa njia ya mtandao na utahusisha kuanzia timu zinazoshiriki ngazi ya wilaya, mkoa hadi taifa.

"Timu zote zinatakiwa kufanya usajili kwa wakati, na ZFF haitakuwa na muda wa ziada kwa ajili ya kuhamisho na usajili," alisema kiongozi huyo.

Ligi Kuu Zanzibar itashirikisha timu 16 ambazo ni pamoja na KMKM, Mafunzo, Kipanga, KVZ, Zimamoto, JKU, Polisi, Uhamiaji, Taifa Jang'ombe, Black Sailor, Mlandege, Malindi, Machomane, Selem View, Yosso Boys na KSFC.

## Geita Gold, Polisi hakuna mbabe

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA na wachezaji wake wapya iliyowasajili kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22, Geita Gold imetoka suluhu dhidi ya Polisi Tanzania katika mechi ya 'kutesti mitambo', iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Geita Gold ambayo imepanda daraja kwa mara ya kwanza utashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara iliwachezesha wachezaji wake wapya akiwamo Benedict Tinoco aliyetokea Kagera Sugar, Oscar Masai, Kelvin Nashon, Daniel Lyanga na Idd Mobby.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi hiyo na kesho wanatarajia kucheza mchezo mwingine dhidi ya Kagera Sugar kwenye uwanja huo huo.

"Lengo ni kuangalia na kutafuta muunganiko wa timu, pamoja na kuangalia mifumo mbalimbali ya uchezaji, mechi hizi zitawaandaa vijana kwa ajili ya kupambana kuelekea msimu ujao," alisema Malale.

Wakati huo huo, kikosi cha Geita Gold kilirejea Geita jana kwa ajili ya kushiriki Tamasha la Geita Day linalotarajia kufanyika leo kwenye Uwanja wa Nyankumbu Girls mkoani humo.

Ofisa Habari wa Geita Gold, Amani Nicolaus, alisema maandalizi ya tamasha hilo yamekamilika na wao watacheza mechi dhidi ya Kagera Sugar.

# Michezo

Jumamosi Septemba 18, 2021

Nipashe




Ronaldo hatacheza mfululizo- Solskjaer

UKURASA 22

# MKWASA AWAPA YANGA MCHONGO

**●●●Ni jinsi watakavyoimaliza Rivers United huku Senzo akitamba...**

**Tunu Hassan na Donald Lukele, TUDARCo**

WAKATI aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, akisema timu hiyo inaweza kupata matokeo chanya na kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mbatha, amesema kikosi chao kiko tayari kwa ajili ya mapambano.

Kikosi cha Yanga kilitarajiwa kuondoka nchini jana usiku kuelekea Nigeria kwa ajili ya mechi ya marudiano dhidi ya Rivers United itakayochezwa kesho kwenye mjini Port Harcourt.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkwasa alisema Yanga inaweza 'kupindua' matokeo endapo benchi la ufundi watafanyia kazi upungufu waliouona katika mechi iliyopita na kuongeza umakini wa hali ya juu kuelekea mchezo huo wa marudiano.

Mkwasa alisema Yanga inatakiwa kuboresha mipango yao ili kuhakikisha wanarudi nchini wakiwa na tabasamu na si matokeo mengine.

"Rivers walimiliki sana mpira wakiwa hapa, hivyo Yanga waongeze tahadhari ya juu kutokana na kasi ya mashambulizi ya wapinzani wao hasa pale wanapokuwa na mpira. Walicheza kama wapo nyumbani na walicheza mchezo wa wazi kabisa, Rivers inauwezo mkubwa wa kukaa na mpira," alisema Mkwasa.

Aliongeza licha ya mechi kuchezwa ugenini, Yanga wanatakiwa waamini katika mpira kila kitu kinawezekana baada ya kubaini mahali ambapo walikosea na kuwapa ushindi wapinzani wao katika mchezo wa kwanza.

Naye nyota wa zamani wa Yanga, Bakari Malima "Jembe Ulaya", alisema timu yake ina nafasi ya kusonga mbele lakini pia akiwataka mashabiki kukubaliana na matokeo yoyote watakayopata hapo kesho.

Malima alisema kikosi chao bado kinahitaji muda wa kujiimarisha kwa ajili ya kufanya vyema kwenye mechi zinazofuata na katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tuwaombee dua wachezaji wapate matokeo mazuri kwenye mechi hiyo, uwezo wakufanya vyema wanao, ila wanayanga pia wapokee kwa mikono miwili matokeo yoyote ya mechi hiyo kwa sababu mafanikio hayaji mara moja, timu nzuri inahitaji muda, mimi ninaamini baada ya msimu huu wa ligi ya ndani kuisha, timu itakuwa nzuri sana sababu ya wachezaji bora waliyopo" alisema Malima.

Senzo alisema tayari wameshaandaa mazingira mazuri ya mahali timu yao itakapofikia lakini wakiwa makini kukwepa aina yoyote ya 'hujuma' kutoka kwa wenyeji wao.

"Nimefika huku tangu Jumatatu na kila kitu kinaenda sawa, mipango yetu inaendelea vizuri, ndiyo maana tumewahi kufika huku ili kujipanga sawa sawa, kwa hiyo tupo tayari kwenye kila idara.

"Kuhusu hujuma huwa zipo tu na haziwezi kukosa, ila tunajitahidi kufanya kila tunaloweza ili tukabiliane nazo, lakini ni vizuri tukasubiri timu ifike kwanza halafu mengine yatafuata," Senzo alisema.

Aliongeza uongozi umefurahishwa na mapokezi kutoka kwa ofisi ya balozi na sasa kilichobakia ni kuipokea timu kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya mchezo huo.

**...MLIMA KILIMANJARO**

Katika hatua nyingine Yanga imeingia makumbaliano na Bodi ya Wizara ya Maliasili ya Utalii kwa ajili ya kutangaza vivutio ya utalii vilivyopo hapa nchini.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, Yanga sasa itaanza kuvaa jezi zenye nembo inayowahamasisha watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani kutembelea Mlima Kilimanjaro na kuzuru Zanzibar.

"Timu yetu ina mashabiki wengi ndani na nje nchi, ni timu inayofuatiliwa sana hata kwenye mitandao ya kijamii, hivyo tunawajibu wa kuungana na serikali katika mambo makubwa inayoyafanya kwa Watanzania wote, tutavaa jezi yenye nembo ya 'Visit Kilimanjaro na Zanzibar', hiyo ni kwa kuanzia, halafu huko mbele tunaweza kuwa na kitu kikubwa zaidi," alisema Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto) na Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hersi Said, wakionyesha jezi mpya itakayotumiwa na timu hiyo katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo itatangaza vivutio vya utalii vya hapa nchini. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yalamba dume kwa ATCL

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesaini mkataba wa miaka miwili na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) wenye thamani ya Sh. milioni 426 kama mshirika wao katika huduma za usafiri wa anga kwa safari za ndani na nje ya nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema jana jijini Dar es Salaam mkataba huo utainufaisha Simba katika maeneo mbalimbali ambayo shirika hilo la ndege la taifa linafanya kazi.

Barbara alisema Simba itakuwa inatoa kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kupata tiketi za safari za ndani na nje kuelekea mahali ambapo timu yao inakwenda kucheza mechi zake.

"Kuendesha timu ni gharama kubwa sana, kupitia makubaliano haya tuliyoingia leo (jana), yanatunufaisha Simba katika safari zetu za ndani na nje ya nchi hasa ukizingatia ni timu ambayo itasafiri sana kwenda nje kucheza mechi nyingi za kimataifa," alisema Barbara.

Naye Mkurugenzi wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema makubaliano hayo yalikuwa ya muda mrefu na sasa yamefikia hatamu kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

"Simba itatumia bidhaa zetu kupitia Air Tanzania kufanya safari zao, hatua hii ni baada ya pande zote mbili kuona kila mmoja ananufaika katika mkataba huo," alisema Matindi.

Wakati huo huo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ezikiel Kamwaga, alisema kambi awamu ya pili ya timu yao imemalizika na kikosi kimerejea jijini tayari kwa ajili ya kushiriki Tamasha la Simba Day.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara watawatambulisha wachezaji wake wapya pamoja na kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), katika tamasha hilo litakalofanyika kesho kwenye Uwanja wa Taifa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 3

9 770856 541002 >